# MADA: SIASA NA UIMARIKAJI WA KISWAHILI KENYA

NA

MUKHWANA, AYUB.

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya 'Master of Arts' Katika Chuo Kikuu Cha Nairobi".

JULAI, 1990

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0146688 7

YALIYOMO


| | | Ukurasa |
|---|---|---|
| Ungamo | | (i) |
| Shukrani | | (ii) |
| Dibaji | | (iv) |
| Sura ya Kwanza | | |
| 1.0 | Utangulizi wa Utafiti | 1 |
| 1.1 | Somo la Utafiti | 1 |
| 1.2 | Malengo ya Tasnifu | 2 |
| 1.3 | Sababu za Uteuzi wa mada | 4 |
| 1.4 | Upeo na Mipaka ya Tasnifu | 7 |
| 1.5 | Mapitio ya Yaliyoandikwa | 7 |
| 1.6 | Msingi wa Nadharia ya Utafiti | 10 |
| 1.7 | Njia za Utafiti | 13 |
| 1.8 | Tanbihi | 14 |
| Sura ya Pili | | |
| 2.0 | Matumizi ya lugha katika Jamii | 15 |
| 2.1 | Utangulizi | 15 |
| 2.2 | Matumizi ya Lugha | 15 |
| 2.3 | Hitimisho | 25 |
| 2.4 | Tanbihi | 27 |
| Sura ya Tatu | | |
| 3.0 | Hali ya Lugha katika Kenya ya Kikoloni | 28 |
| 3.1 | Utangulizi | 28 |

3.2 Sera ya Lugha Kenya Enzi wa Waingereza 29

3.3 Tathmini ya Hali ya Lugha Kenya ya Kikoloni 42

3.4 Hitimisho 51

3.5 Tanbihi 53


Sura ya Nne


4.0 Hali ya Lugha Kenya Baada ya Uhuru 56

4.1 Utangulizi 56

4.2 Kiingereza na Uimarikaji wa Kiswahili 57

4.2.1 Msingi wa Athari za Kiingerza kwa Uimarikaji wa Kiswahili 57

4.2.2 Elimu na Uimarikaji wa Kiingereza dhidhi ya Kiswahili 60

4.2.3 Uchumi na Uimarikaji wa Kiingereza dhidi ya Kiswahili 61

4.2.4 Urasmi wa Kiingereza na Uimarikaji wa Kiswahili 64

4.3 Lahaja za Kiswahili na Uimarikaji wa Kiswahili 68

4.3.1 Vita vya lahaja Muhimu Uswahilini 68

4.3.2 Kiunguja na Maslahi kwa Waongeaji wake 70

4.4 Athari za Sheng' katika Kiswahili 72

4.4.1 Nadharia zihusuzo Chimbuko la Sheng' 72

4.4.2 Sheng' na Uimarikaji wa Kiswahili 75

4.5 Hitimisho 77

4.6 Tanbihi 78

Sura ya Tano

5.0 Hitimisho 81

Bibliografia 84

UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine cho chote".

MUKHWANA, AYUB
(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii walioteuliwa na Chuo Kikuu".

DAKTA JAY KITSAO

MWALIMU KITHAKA wa MBERIA

## SHUKRANI

Katika kazi hii nimejaribu kujitokeza na picha ya hali ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Ikiwa nimefaulu ni kwa sababu ya misingi imara ya Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Idara hii imeniathiri katika fikira zangu na kwa hivyo sina budi kuwashukuru wote waliomo: wahadhiri kwa wanafunzi. Hasa ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu - Dakta Jay Kitsao na Mwalimu Kithaka wa Mberia - kwa mashauri yao ambayo kama singeyazingatia kazi hii haingekuwa hivi ilivyo. Pia ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu Bi. Shitemi, Bi. Rayya, Bw. karanja, Bw. Mbatia, Bw. Lukorito, na Bw. Kulundu kwa kunipa moyo wa kuendelea kuishughulikia kazi yangu katika wakati wa uvunjifu mkubwa. Shukrani za kidhati pia zimwendee mwanafunzi mwenzangu Mwalimu Mgullu ambaye amenifaa sana kwa kuniletea data kutoka Tanzania.

Nimerejelea kazi mbalimbali zinazoongelea nyanja ya maendeleo ya lugha. Kwa sababu hii, nawashukuru waandishi niliowarejelea na kusema kuwa ikiwa kazi hii imefaulu ni kutokana na maandishi yao. Hata hivyo, endapo kuna mahali palipoenda kombo ninabeba lawama zote. Lakini nasisitiza kuwa bila wao kazi hii isingekuwa namna ilivyo.

Ningependa pia kumshukuru mwalimu na rafiki yangu mkuu Dakta Walter Nabakwe wa Idara ya Filosofia ya Chuo Kikuu Cha Nairobi kwa fadhila alizonifanyia kwa kunipa makazi wakati nilipokuwa nimeingiliwa na wanyang'anyi katika mtaa wa Kangemi. Na mwisho, namshukuru mpiga taipu Bi. Sarah N. M. Kamau kwa kazi yake nzuri. Kwa wale wote nasema Ahsanteni na Mungu akulindeni.

DIBAJI

Kazi hii ilihitaji kukabiliwa na wasiwasi na uoga fulani kwa namna ambavyo mada iliyoshughulikiwa inaweza kusisimua hisia katika miili ya watu fulani na pia kwa jinsi ambavyo ni tatanishi. Tumewajibika kujitokeza na fasiri mbalimbali kuhusi- ana na upangaji wa lugha nchini Kenya. Katika kufanya hili, imetubidi kuyataja baadhi ya masuala ya kijamii ambayo hayange- weza kuzuilika katika kazi kama hii. Ni fikira zetu kwamba hatukufasiri vibaya matukio mbalimbali ya kilugha au malengo ya wapangaji lugha nchini Kenya.

Tasnifu hii imegawika katika sehemu tano. Sehemu ya mwanzo ni Utangulizi wa kazi nzima. Sehemeu ya pili inahusu yale masuala ya kilugha ambayo kwa njia moja ama nyingine yanaingiliana na tasnifu hii. Inaeleza na kujadili dhana fulani muhimu kuhusu lugha, mbali na kuwa inajadili uhusiano ulioko baina ya kuimarika kwa lugha na masuala mengine ya kijamii kama vile utawala. Sehemu ya tatu pamoja na ile ya nne ni sura ambazo, zikitumia yaliyosemwa katika sehemu ya pili, zinahakiki lugha katika Kenya. Sehemu ya tatu inazungumzia Kenya ya kikoloni ilhali ile ya nne inaongelea Kenya huru. Halafu sehemu ya mwisho ni Hitimisho la kazi nzima. Katika sehemu hii wasomi wamepewa mapendekezo ya nyanja zilizo na mafungamano fulani na kazi hii na ambazo zinaweza kutafitiwa katika siku za usoni.

Kijumla, ni imani yetu kwamba tasnifu hii itawapa wanafun- zi na wasomaji wengine wa Historia ya lugha ufahamu mwema wa namna'uwezo' walio nao wanasiasa unavyoweza kuathiri historia na maendeleo ya lugha fulani.

SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi wa Utafiti

### 1.1 Somo la Utafiti

Watu fulani wanapoipa lugha fulani umuhimu mkubwa kuliko ule upewao lugha nyingine hili linakuwa dhibitisho la tabia za watu hao au la muundo wa jamii wanamoishi. Ikiwa jamii fulani itachambuliwa ili kuudhihirisha ukweli huu, wanajamii inayohusika watafaidika kwa namna watakavyofahamikiwa na kwa nini kutumia lugha fulani humfanya mtu ajiambatanishe na watu fulani katika jamii. Lugha anayoitumia mtu kwa kuwasiliana na wenzake inaweza kumfanya aeleweke zaidi katika muktadha fulani hata bila kuzingatia kile anachokiongelea. Hii ni kwa sababu tofauti katika lugha wanazozitumia watu wawili ni dhihirisho la waliko watu hao katika ngazi za kijamii.

Tumetafiti hali na matumizi ya lugha nchini Kenya. Kwa kuwa utafiti kuhusu lugha hauwezi kutenganishwa na jamii, maana mahusiano ya kilugha ni mahusiano ya kijamii vile vile, tumetafiti usambamba ulioko baina muundo wa jamii na muundo wa lugha nchini Kenya. Yaani tumechunguza ikiwa kule kuchagua lugha fulani itumike mahali fulani na watu fulani hufanywa ili kuathiri muundo wa jamii inayohusika ili kutosheleza mahitaji fulani ya kijamii.

Katika tasnifu hii msisitizo utakuwa katika mwingiliano wa muundo wa kijamii na muundo wa kilugha nchini Kenya na jinsi ambavyo miundo hii huathiriana. Kimsingi, tumetafiti juu ya usambamba ulioko kati ya lugha wanayoitumia watu fulani na muundo wa jamii huku tukizitia maanani shida za tofauti za kijamii na mabadiliko ya nchi ya Kenya kihistoria. Yote haya tumeyatia katika mkabala wa kisiasa ili kueleza ni kwa jinsi gani sera ya lugha nchini Kenya imeathiriwa na siasa.

## 1.2 Malengo ya Tasnifu

Nchi ya Kenya ina Kiswahili kama lugha yake ya Taifa. Lugha hii yazungumzwa na kueleweka kote nchini. Pia kunazo lugha nyingine nyingi za kienyeji (mbali na Kiswahili) pamoja na zile zilizo za kigeni. Lugha za kigeni nchini Kenya ni matokeo ya maingiliano ya miaka mingi kati ya Kenya na nchi za kigeni. Kwenye mstari wa mbele, miongoni mwa lugha za kigeni zote, ni Kiingereza.

Hali hii ya kuwa na lugha nyingi ni ithibati-tosha kuwa Kenya ina utajiri wa lugha. Lakini, lugha hizi hutofautiana katika hadhi ya kutumika kwazo kama vyombo vya mawasialiano. Tofauti ya hadhi na nafasi ya kila mojawapo ya lugha hizi huwa ni suala la kisiasa maana lugha ni suala la kijamii, na kama masuala mengine ya

kijamii lugha haiwezi kutenganishwa na siasa. Hii ni kwa sababu sera zo zote zile huwa na makusudio fulani ambayo yanapotekelezwa huathiri mifumo yote ya maisha ikiwemo ile ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tasnifu hii basi ina malengo yafuatayo:

(i) Kurejelea historia ya lugha nchini Kenya, japo kwa ufupi, na kufafanua nafasi, hadhi, na mipaka ya matumizi ya lugha mbili kuu nchini Kenya: Kiingerreza na Kiswahili, na kueleza kuwa hali hii haitokei tu kwa sababu lugha na siasa ni masuala yanayofungamana na kuandamana bali kuwa ni wazungumzaji walio muhimu katika kuimarisha lugha na wala si hali za kiuchumi za wazungumzaji hao;

(ii) Kutambua baadhi ya makusudio muhimu waliyokuwa nayo wakoloni wa Kiingereza katika kuwa na aina ya sera ya lugha waliyokuwa nayo nchini Kenya na kuonyesha jinsi yalivyoanzishwa na kutekelezwa. Hivi, tutadokezewa namna ambavyo Wakenya wanaweza kuzirutubisha sera zao kuhusu lugha watakayoitaka. Hapa tunatafiti hoja kuwa Kiswahili hakikuendelea na hakitaendelea na kuimarika maana kiliwekewa na kinawekewa vikwazo na vizuizi vingi na wanasiasa;

(iii) Kutafiti ikiwa sera ya lugha ya wakoloni wa Kiingereza nchini Kenya imekuwa na athari zinazoendelea kuhisika katika sera za sasa za nchi hiyo kuhusu lugha, kwa kurejelea hasa

Kiswahili. Hoja hii ni muhimu maana itatuwezesha kujua jinsi sera za sasa kuhusu lugha nchini Kenya zilivyo tofauti na zile za kikoloni licha ya kuweza kujua athari za wakoloni hawa kwa Wakenya, na hivi tutaweza kusema ni kwa kiasi gani Kenya huru imekengeushwa kilugha. Tunalenga katika kusema kuwa Kenya huru ni tofauti na Kenya ya kikoloni kilugha;

(iv) Kufafanua haja na umuhimu wa kukuza lugha ya Kiswahili maana ni chombo muhimu cha mawasiliano nchini Kenya. Hivi tutaeleza kuwa lau Kiswahili hakikufanyiwa juhudi za kimakusudi za kukikuza, kitajifia kwa kukosa msukumo kutoka kwa serikali ya Kenya.

## 1.3 Sababu za Uteuzi wa Mada

Ijapokuwa tunatambua kuwa idadi kubwa ya Wakenya yajua umuhimu wa Kiswahili na kuwa sehemu kubwa ya sera za serikali yafaa itie maanani matakwa yao kilugha, tunafikiri ni muhimu zaidi kutambua na kuainisha yale yaliyofanywa na yanayofanywa ili kukiendeleza Kiswahili. Hivi kila awamu ya historia ya Wakenya itapewa nafasi yake kulingana na yale iliyofanyia lugha ya Kiswahili.

Hali hii yazushwa na hoja kuwa kitu cho chote ambacho ni muhimu katika maisha ya binadamu kama

ilivyo lugha, huhitaji kushughulikiwa kwa makini makubwa zaidi. Hii ni kwa sababu ufanya-kazi wake utaweza kueleweka na hata kuwasaidia watumizi wake kujielewa. Kwa hivyo tumeichagua mada hii ili kuangaza lugha ilivyotumika (na inavyotumika) nchini Kenya katika muktadha wake wa kihistoria.

Hali hii yatokana na hoja kuwa lugha, mara nyingi, hufanya kazi kulingana na matakwa ya jamii maana jamii hutegemea lugha kwa mahusiano ya watu wake. Yaani ni busara kusema kuwa kukua kwa lugha na kufanya kazi kwake katika jamii kwa kipindi fulani cha kihistoria ni mambo yanayohusiana na kufungamana. Hali hii imekuwa ikitazamwa na wengi wetu kama kwamba ni jambo la kawaida kuhusu lugha ya Kiswahili. Basi tumechagua mada hii ili kuikosoa jamii ya Kenya na labda ulimwengu kwa jumla kuwa nafasi ya Kiswahili nchini Kenya ni suala lililo na misingi yake katika watumizi na matumizi ya lugha hii.

Kenya ilipata uhuru mwaka 1963. Lakini kama inavyofahamika, kule kujipatia uhuru kwa mataifa ya Kiafrika kulikuwa ni mwanzo tu wa safari ndefu ya kujikomboa. Safari hii ilihusu, miongoni mwa mambo mengine, uhuru wa kitamaduni. Basi sababu mojawapo ya kuchagua mada hii ni kutafiti jinsi ambavyo Kenya imejikomboa kiutamaduni kwa kurejelea kipengele cha

lugha. Hivi tutapata tofauti iliyoko katika sera za lugha katika enzi ya wakoloni wa Kiingereza na zile za Kenya huru. Hii ni kwa sababu katika enzi ya ukoloni, lugha ya matumizi ilitegemea wale wenye majina na vyeo. Lakini sasa ambapo nchi za Kiafrika zimejinyakulia uhuru, yamejitokeza maendeleo mapya katika siasa. Nchini Kenya maendeleo haya ni katika siasa yenye misingi ya demokrasia. Katika maendeleo haya yategemewa kuwa kuna uhusiano kati ya raia na watawala; uhusiano ambao huzalisha hali iitwayo 'ya uwakilishaji'. Basi tumeiteua mada hii ili kutafiti ni kwa jinsi gani sera ya lugha nchini Kenya baada ya uhuru hutegemea walio wengi katika jamii kwa kuzingatia hoja kuwa

> Katika jamii iliyogawanyika kilugha kushiriki lugha moja kunaweza kuwa kama nyenzo ya umoja, chombo cha kurahisisha maendeleo ya kiuchumi, na ishara ya utaifa.[2]
>
> (Tafsiri Yetu)

Ni machache sana yajulikanayo kuhusu namna uwezo alionao mtu waweza kuathiri mawasiliano nchini Kenya. Hali hii yaweza kuelezwa kihistoria na kisiasa. Basi, sababu mojawapo ya uteuzi wa mada hii ya utafiti ni kueleza jinsi wakoloni, (na ambao walikuwa na uwezo wa kisiasa, kiuchumi, na kijamii) waliwalazimishia Wakenya njia fulani za kuwasiliana.

## 1.4 Upeo na Mipaka ya Tasnifu

Kazi yetu, kama tulivyokwisha kueleza, ni uchambuzi wa hali ya lugha nchini Kenya kwa kuegemea nafasi ya Kiswahili. Kwa hivyo tumejikita zaidi katika lugha hii.

Mada 'Siasa na uimarikaji wa Kiswahili Kenya' yaweza kufasiriwa kwa njia kadhaa. Katika kazi hii ina maana ya maamuzi ya watu (au vikundi vya watu) walio na majukumu ya kiutawala na ya kisheria kiasi kwamba yale wanayoyasema au kuyatenda kuhusu lugha yanakuwa na athari fulani hata kwenye ngazi za kitaifa. Tunajihusisha hasa na yaliyofanywa kuhusu lugha katika mianda mbalimbali ya kijamii - hasa ule wa elimu - na kuihusisha na siasa. Hata hivyo tabia za watu fulani katika jamii pia zaweza kuambatishwa na athari fulani za kisiasa. Basi tumeshughulikia suala la usanifishaji wa Kiswahili pamoja na lile la kuzuka kwa Sheng' na jinsi yanavyoathiri kuimarika kwa Kiswahili.

Muda tunaoushughulikia ni baina ya mwaka 1900 na sasa, ingawa kwa sababu ya uhitaji na mkamatano mwema wa hoja tunaweza kurudi nyuma kidogo.

## 1.5 Mapitio ya Yaliyoandikwa

Alexandre, P (1972) amezungumzia hali ya lugha barani Afrika. Anaitalii hali hii ilivyokuwa kutoka

mwanzo wa enzi ya wakoloni wa Kizungu hadi wakati baadhi ya nchi za Afrika zilipoanza kujinyakulia uhuru wa bendera. Kwa kuwa Afrika ni kubwa, ina lugha nyingi, na kuna mengi yanayoweza kusemwa kuhusu kila lugha, Alexandre anatajataja tu mambo muhimu kuhusu lugha hizi katika pitepite zake. Jambo linalomshangaza ni hali ya kugawanyika kwa mataifa ya Afrika kilugha miongoni mwa yale yanayozungumza Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu (1972:81). Kuna mambo mengi yaliyosababisha hali hii na mojawapo ni sera za wakoloni hawa.

Baadhi ya mambo anayozungumzia Alexandre yanaingiliana na baadhi ya yale tuliyozungumzia. Hivi basi Alexandre ametuchangia katika kazi yetu maana tumeyachukua [illegible] yanayoingiliana na mada yetu ya utafiti, tukayatathmini na kisha kuyatia yafaapo katika mkururo wa sura za kazi hii.

Bakari, M (1978) amesema kuwa ufufuzi wa utamaduni huenda sambamba na mwamko walio nao watu kisiasa. Anatoa mfano wa nadharia ya Uzayoni ambayo anasema kuwa kwa Waisraeli ilikuwa na maana ya kuwaza Kiyahudi, kurejea Israeli na pia kujifunza Kihebrania hata baada ya mtu kutimiza miaka tisini. Bakari anaendelea kusema kuwa hata masomo yao ya shuleni yalifunzwa katika Kihebrania na hali hii iliipa lugha hii misingi imara kama lugha ya kisasa. Kwa

sababu hii, anajaribu kulinganisha ufanifu wa sera ya lugha ya Israeli na ya Kenya. Ijapokuwa anatoa mifano ya lugha mbalimbali nchini Kenya katika kutilia nguvu anayoyasema, yale aliyoyasema kuhusu Kiswahili yamekuwa na umuhimu mkubwa katika kazi yetu.

Mutahi, K (1977) anapitia sababu zilizosababisha kuwako kwa hali ya sasa ya lugha nyingi (za kutumia kwa mawasialiano) nchini Kenya. Katika kufanya hili, anatazama hali ya lugha nchini Kenya kabla ya kuja kwa wakoloni mpaka baada ya miaka ya 1960. Kwa kuwa eneo alilopitia ni pana, amekosa kujadili baadhi ya masuala kwa kina ambacho yanastahili katika kurasa chache alizoziandika. Hata hivyo, makala haya yake yametumulikia kazi yetu - hasa kabla ya Kenya kujipatia uhuru.

Sindiga, I (1977) anaangalia sababu ambazo zimefanya hali ya lugha nchini Kenya kukosa kuwa na usare, huku akirejelea hasa Kiswahili baina ya mwaka 1900 na wakati wa uhuru. Anayoyasema Sindiga yana mengi yanayoingiliana na mada yetu ya utafiti na kwa hivyo tunatumai yametufaa si haba pale tulipoyatia katika mkabala wa kisiasa.

Whiteley, W (1969 na 1974) ameandika mengi ambayo yanazungumzia hali, hadhi, nafasi na uimarikaji wa Kiswahili. Aliyoandika yametufaa maana tumeyachambua kwa mujibu wa matakwa ya msingi wa nadharia yetu ya utafiti na kujua mahali pa kuyaweka. Watu wengine waliolishughulikia suala la uimarikaji wa Kiswahili kwa kulihusisha na siasa katika pitepite zao, au hata kwa kulitaja tu ni pamoja na Gorman, T.P. katika W. Whiteley (1974;394 - 453), Massamba, D.P.B. (1987; 180 - 191), na Ngugi wa Thiong'o (1981). Tumezifinyanga kazi hizi zote ili ziingiliane na mada yetu ya utafiti na ni matumaini yetu kuwa tumejitokeza na kazi yenye kina na iliyozama zaidi ya zote.

## 1.6 Msingi wa Nadharia ya Utafiti

Wasoshalisti, kuanzia Mtakatifu Simon mpaka Marx, waliihusisha dhana ya maendeleo na matakwa ya matabaka. Kwao, maendeleo katika masuala ya kijamii hayakuwa ni masuala ya kuishughulisha jamii nzima bali tabaka mojawapo katika jamii inayohusika. Kwa kutizama maendeleo kama suala la kitabaka, Marx alijitokeza na kuuona uchumi kuwa ndio uti wa mgongo wa maendeleo na kwa hivyo akasema kuwa daima kuna mkinzano katika jamii kuhusu ni nani amiliki uchumi na kwa kutumia nyenzo gani.

Lugha ni mojawapo ya nyenzo hizi. Na ili kuelewa hali ya lugha nchini Kenya kutoka enzi ya wakoloni wa Kiingereza hadi sasa, yatupasa kuangalia harakati za kitabaka ambazo zimekuwako pamoja na nyenzo za uzalishaji mali. Hili laweza kufanywa kwa kuielewa historia ya sera za lugha nchini Kenya kwa kuirejelea nadharia ya ki-Marx. Nadharia hii inapinga uhalalishaji wa maovu ya aina yo yote ile katika jamii kwa kutumia chombo cho chote kile. Nadharia hii, kwa kuwa ina misingi yake katika uchumi, hujaribu kumulika chanzo cha umaskini, unyonge na unyonyaji katika jamii na hujitokeza kama mtetezi wa walio wengi dhidi ya wachache walioshika hatamu za uongozi. Nadharia hii ya ki-Marx huyaangalia maisha ya binadamu kwa kurejelea yaliyopita, yaliyopo na yajayo. Kwa kuwa upeo wa tasnifu yetu wahusu athari za siasa kwa Kiswahili nyakati za ukoloni wa Mwingereza hadi sasa ni matumaini yetu kuwa nadharia hii imetufaa zaidi.

Isitoshe, hali ya lugha ilivyokuwa tangu nyakati za wakoloni wa Kiingereza nchini Kenya hadi hivi leo imeathiriwa sana na hali halisi ya uzalishaji mali. Katika wakati wa ukoloni huo lugha ya Kiingereza ilikuwa ndiyo yenye hadhi maana ilikuwa ndiyo lugha waliyoitumia watawala na ambao pia ndio walioumiliki uchumi wa Kenya. Lugha za kienyeji,

kikiwemo Kiswahili zilikuwa ni za mawasiliano ya kiwango cha kikabila, na hapa na pale kitaifa.

Baada ya Kenya kujipatia uhuru, hali hii ilichukuliwa vivyo hivyo maana utamaduni wa Mwingereza (na wa kikoloni mamboleo kwa jumla) uliendelezwa; na kwa hivyo lugha ikiwa mojawapo ya vipengele vya utamaduni, haikufanyiwa mageuzo mengi. Sera ya lugha inayowapa watu shuruti kuhusu lugha gani izungumzwe lini na wapi huenda sambamba na mfumo wa kiuchumi na kisiasa. Kama ilivyokuwa katika enzi ya ukoloni wa Mwingereza, hivi leo wale wenye kuzungumza Kiingereza Kenya eti ndio 'wenye nacho' na wale wenye kuzungumza Kiswahili - ambayo ni lugha inayowaunganisha wafanya kazi na mafalahi - ndio 'wasinacho'.

Hali hii, kama inavyojadili nadharia ya Ki-Marx, hugawa watu katika matabaka na ndiyo yenye kuathiri mfumo wa lugha nchini Kenya. Jambo ambalo tunadadisi, kwa kuitumia nadharia hii ya Ki-Marx ni jinsi ambavyo kutokukua kwa Kiswahili kunaweza kuelezwa kwa kuzingatia hali ya kiuchumi na kisiasa nchini Kenya huku tukizingatia hoja kuwa uwezekano wa kuwako kwa mikinzano ya kitabaka huenda iliathiri - labda vikubwa - harakati za uundaji sera.[3]

## 1.7 Njia za Utafiti

Suala la sera ya lugha nchini Kenya limeshughulikiwa na watu kadhaa. Wengine wamelishughulikia katika muktadha wa mataifa yote matatu ya Afrika Mashariki ilhali wengine wamelitazama suala hili la lugha kwa kurejelea mataifa yote huru ya Afrika. Watu wengine nao wamelitazama kama jambo jumuishi na kwa hivyo kwa kutalii hali ya lugha katika taifa fulani linaloendelea wakasema hali hiyo ndiyo iliyo katika mataifa mengine ya Ulimwengu wa Tatu pasi na kujali mipaka ya mabara. Basi, mradi suala la sera ya lugha limeshughulikiwa na wengi, na pia tafiti nyingi zifanywazo siku hizi - ziwe za kisayansi au za nyanja nyingine yo yote ile - hurejelea maktaba, shughuli zetu nyingi kuhusu mada hii zimekuwa katika maktaba.

Licha ya kuwa tumesoma katika maktaba, imetubidi kwenda nyanjani ili kuhoji wataalamu wa suala hili la sera ya lugha, pamoja na wazee walioshuhudia baadhi ya majadiliano kuhusu suala la lugha nchini Kenya katika nyakati za ukoloni na pia zile za Kenya huru.
Pia tumehoji sehemu ya umma wa Kenya ili kupata maoni yao kuhusu Kiswahili. Baadhi ya maswali ambayo tumeuliza yamehusu fikira zao kuhusu kufanywa kwa Kiswahili lugha ya mawasialiano kote nchini Kenya, kujitosheleza kwa Kiswahili kama chombo cha mawasiliano, n.k. Hivi tumeweza kujua ni kwa jinsi

gani suala la lugha ya Kiswahili nchini Kenya ni la kisiasa au la kihisia tu.

Hizi njia mbili ndizo ambazo tulikusudia na tumetumia katika utafiti wetu lakini hatukutaka kujifunga kwazo maana kama njia nyingine ingetokea natuione kuwa ingetufaa kwa kuongezea kazi yetu malighafi na hata kuiboresha, hatungesita kuitumia.

## 1.8 Tanbihi

1. Tazama Rose, R (1964) katika Politics in England: An interpretation, Little, Brown and Co., Boston uk.103-5.

2. Cooper, R. L. (?) katika makala yaitwayo "Government Language Policy" katika Language in Ethiopia, M.L. Bender (Mhariri) uk.187

3. Haya ni maneno ya Carrier na Kendall katika Social Policy Studies na yaliyonukuliwa na A. Pemberton katika 'Politics and History' - Australian Journal (1984) uk.57

## SURA YA PILI

## 2.0 Matumizi ya Lugha katika Jamii

### 2.1 Utangulizi

Taathari za kisiasa, kijamii na kiuchumi ambazo zimeungana ili kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa jinsi ilivyo ni muhimu katika kutuwezesha kuielewa zaidi hali ya sasa ya lugha hii na hata hali itakavyokuwa siku zijazo. Lakini kabla ya kuzijadili taathira hizi ni muhimu kupitia baadhi ya mambo yanayoweza kufanywa na lugha ili yawe ni msingi wa yale yatakayosemwa kuhusu chanzo na maendeleo ya taathira hizi. Tutakayoyasema hapa yatakuwa kama mhimili wa sura zitakazofuatia.

Ikumbukwe kuwa uhusiano baina ya lugha na wazungumzaji ni kwamba hautenganishiki. Ni kwa sababu hii ndipo ukiwatoa watu mahali fulani, basi lugha inakuwa haipo tena maana lugha hupewa umuhimu wake kutokana na wazungumzaji wake. Ni kutokana na hali hii ndio utakuta kwamba baadhi ya lugha zasomeshwa kwingi ulimwenguni na wala si nyingine.

### 2.2 Matumizi ya Lugha

Matumizi ya lugha hayawezi kueleweka barabara bila ya kwanza kujua chimbuko la lugha kwa kujibu maswali haya: Mbona lugha ikazuka?, na, Lugha ilizukaje?

Wachunguzi huhitilafiana na kutofautiana katika kueleza chanzo cha lugha. Watu wenye imani katika dhana kuwa mambo yote hutoka kwa Mungu watadai kuwa lugha iliteremshiwa wanadamu wa mwanzo na Mwenyezi Mungu alipowaumba. Wanasayansi nao wana mtazamo wa kiuyakinifu juu ya asili ya lugha na wanaeleza kuwa chimbuko la lugha lilihusiana na maendeleo ya binadamu katika utengenezaji, na hasa utumiaji wa zana za kazi. Ingawa mambo yaliyofanya lugha ichimbuke yana historia ndefu, jambo la kukumbukwa ni kwamba kulitokea uhitaji wa kupashana habari kuhusu shughuli za kila siku za watu ndipo lugha ikazuka.

Lugha haina umuhimu wa kupashana habari tu maana kuna umuhimu mwingine mwingi. Tukumbuke kuwa

> Lugha, kama wote wanavyojua, ni sura ya kipekee inayomtambulisha mwanadamu. Ndiyo msingi wa maingiliano kati ya watu na ndicho kitu kikuu kinachowaunganisha watu katika makundi. Huwapa wanadamu utambulisho na hali ya kuhisi kwamba ni watu wa mahali fulani. Lugha huwawezesha watu kushirikiana kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wote.[1]
>
> (Tafsri Yetu)

Pia ni vyema tukumbuke kuwa

> kwa mtu kuzungumza lugha fulani na wala si nyingine ni tendo la kiada, ni maelezo kuhusu

> hadhi ya mtu huyo; kuzungumza lugha moja na majirani zako ni dhihirisho la umoja ulioko kati yako na hao majirani zako, kuzungumza lugha tofauti na ile wanayoiongea majirani hudhihirisha utengano wa kijamii au hata uhasama ulioko.[2]
>
> (Tafsiri Yetu)

Nuku hizi mbili zaendeleza hoja kuwa lugha yaweza kutumiwa kwa minajili ya kuwaelewa wanajamii fulani kifikira kutokana na tabia zao za lugha.

Osundare, (1981:96) akimnukuu Franz Fanon katika <u>Black Skin, White Masks</u> anafafanua zaidi juu ya matumizi ya lugha anaposema

> kuzungumza kuna maana ya kuweza kutumia sintaksia fulani, kuelewa mofolojia ya lugha hii au ile, lakini juu ya yote kubobea katika utamaduni, kuunga mkono umuhimu wa ustarabu.
>
> (Tafsiri Yetu)

Akitoa maelezo zaidi juu ya haya anayoyasema Fanon Osundere asema

> Lugha yaweza kutumika kunyanyasa, kufunga, kumdunisha mtu katika utu wake, kumwekea mtu mipaka, na kumtenga. Yaweza kuwa chombo cha kuendelezea maslahi ya wenye navyo, na cha kuwanyamazishia wanyonge.[3]
>
> (Tafsiri Yetu)

Kutokana na nukuu hizi tunaweza kusema yafuatayo, kuhusu matumizi ya lugha katika jamii. Kwanza, lugha ndicho chombo kibebacho utamaduni wa wazungumzaji. Watu fulani wanapolazimishiwa lugha fulani ya kigeni huwa wamelazimishiwa utamaduni wa wageni hao pia. Hii ni kwa sababu kila neno la lugha analojifunza mtu huwa limebeba chembe za utamaduni wa watu hao. Ni kutokana na hali hii ndio A. A. Mazrui, (1975:185) anasema kuwa ni jambo lisilo la kawaida kutenganisha lugha na utamaduni maana mtu hawezi kujifunza vyema kuhusu utamaduni wa Wafaransa kwa kutumia Kihindi au Kiarabu. Ili mtu kupata utamaduni wote wa Wafaransa lazima utamaduni huo umfikie kwa matumizi ya Kifaransa maana fikira za watu na lugha wanayoiongea ni mambo yaliyofungamana. Ni kwa sababu hii ndipo utakuta kuwa

> ... Baadhi ya wazungumzaji watahitari kuzungumza katika lugha zao za asili hata wanapokuwa wanauhutubia umati ulio na watu wa makabila mbalimbali maana wanaweza kujieleza waziwazi zaidi katika lugha zao na wanaweza kuelezea moja kwa moja utamaduni watakao kuuzingatia. Tafsiri katika lugha nyingine kila mara huwa na kasoro. Ni kwa sababu hii ndipo lugha yasemekana kuwa ni chombo cha kuelezea utamaduni wa watu fulani, kwa kuwa utamaduni wenyewe umebebwa na lugha ya watu hao[4].

(Tafsiri Yetu)

Mbali na kuwa lugha hubeba utamaduni wa watu, chombo hiki pia huueleza. Hii ni kwa sababu kule kujua lugha fulani humfanya mtu azijue pia chembe fulani za utamaduni wa waongeaji wa lugha inayohusika. Kila neno la lugha analoliongea mtu huwa ni kifaa cha kumfunza kuhusu mazingira yake na jinsi binadamu anavyoyakabili katika harakati zake za kujiendeleza. Kwa mfano, mtu anayekifahamu Kiingereza anaposema

<u>Sirengo has taken a French Leave</u>

anakuwa anatudokezea kitu fulani kuhusu namna Waingereza wanavyowatazama Wafaransa kwa jinsi wanavyojiondokea mahali.

Pia lugha kama chombo cha utamaduni humwezesha binadamu kuwa na mtazamo fulani kuhusu ulimwengu huu tuishimo, mbali na kuwa lugha pia huathiri mambo ya kuthaminiwa na kutothaminiwa katika jamii. Hali hii humsaidia binadamu kuielewa dhana ya maisha na nafasi yake (yeye) katika jamii aishimo. Yaani lugha ni kama kibali cha uanachama katika jamii mbali na kuwa ni ishara ya hadhi katika daraja za kijamii. Kimsingi, lugha kama kifaa kibebacho utamaduni husaidia katika kuipa jamii fulani na wanajamii hiyo mwelekeo fulani wa kijamii ambao unaiwezesha jamii yenyewe kusemekana kuwa ni tofauti na nyingine hata kama zote ziko katika eneo moja la kijeografia.

Kutokana na hali hii, tunaweza pia kusema kuwa lugha hutumiwa ili kuleta umoja katika jamii fulani. Katika lugha kuifanya jamii kuweza kujitambulisha, inaiunganisha na kuifanya ijihisi kama inayothamini mambo mamoja, jinsi moja za kujiendelezea maisha, n.k. Yaani lugha hufufua na wakati huo huo ikasisimua hisia za muungano wa kikabila au kitaifa pale inapojitokeza na kujidhihirisha kama chombo cha umoja miongoni mwa wazungumzaji wake. Kwa sababu hii si ajabu kuona lugha ikitumiwa ili kuchochea hisia za watu kusudi wajihisi kuwa ni wamoja au walio katika tabaka moja. Hapa lugha inajitokeza kama chombo kinachopigania kutokuweko kwa usawa katika jamii na wakati huo huo kama chombo cha kuiunganisha jamii kwa kuonyesha umoja wa kitamaduni na (kwa) kumkaribisha msikilizaji aje kujitambulisha na tajriba ambayo wenzake wamo.

Lugha pia hutumika na watu ili kuhalalisha nafasi zao katika jamii. katika jamii iliyogawanyika kimatabaka, watu wote hawatumii lugha moja; hata wakitumia lugha moja kutakuwa na tofauti katika matumizi ya lugha hiyo hiyo moja. Ni kwa sababu hii ndipo dhana kama vile Queen's English na Black American English zikazuka. Hali hii yatokana na ukweli kuwa pale lugha zaidi ya moja inapotumiwa katika shughuli za kielimu si elimu yote wapatayo watu iliyo na umuhimu sawa au thamani sawa. Hii ni kwa sababu aina za kazi wazifanyazo watu na uwezo wa kisiasa walio nao ni

mambo mawili yanayofungamana, na ambayo yanakuwa si sawa kote katika jamii fulani kutokana na tofauti za kielimu na kiujuzi. Yaani kunakuwa na juhudi za kima-kusudi ambazo huhakikisha kuwa ni watu fulani tu ambao watapata ujuzi wa aina fulani.

Ni katika hali hii ambapo matabaka yenye uwezo huwa walezi wa ujuzi wa aina hii, huku wakijichukulia majukumu ya kuwapangia wengine sheria. Basi wao huwa katika nafasi nzuri ya kuweza kutoa vigezo vya kufaa na kutofaa kwa mambo katika jamii. Na ili mtu aliye katika tabaka la chini kusonga mbele na kuingia katika tabaka lile jingine, huwa akiwekewa sheria, vizuizi na vikwazo mbalimbali kama vile mitihani. Kama mtu hakupita mtihani fulani basi inakuwa ni yeye mwenyewe wa kujilaumu. Vikwazo hivi hutumiwa tu ili kuhalalisha nafasi za wale wenye navyo'. Katika hali hii, mbali na kuwa lugha hugawia watu mipaka yao ya kielimu na kiujuzi, pia lugha hujitokeza na miundo ya lugha kutegemea ujuzi wa mtu fulani.

Hapa tunajaribu kujibu swali moja muhimu ambalo ni: Je, ni mambo gani ya kisosholojia ambayo huathiri matumizi ya lugha katika jamii? Tumeeleza kuwa mwanzo wake ni hali ya kuwa na matabaka katika jamii.

Muundo wa kimatabaka huathiri elimu na kazi za watu, na wakati huo huo kuwapa wanajamii mahusiano fulani huku hali hii ikiyapa maisha yao sura ambazo hulitambulisha tabaka lao kama lililo lao huku zikilitofautisha na lile lisilo lao. Hali hii ya kuwapa watu fulani maslahi ambayo wengine hawapati huweka mipaka ya aina fulani kati ya wanajamii huku ikiwapa baadhi ya wanajamii hadhi ya juu dhidi ya wengine. Kwa hakika, ni utovu wa mantiki kufikiri kuwa tofauti hizi zilizo na misingi katika walivyo navyo watu' haziwezi kuathiri hali zote za maisha ya watu, ikiwemo lugha. Basi lugha husababisha hali ya kuwa na mpaka kati ya wenye nguvu na wanyonge, matajiri na maskini katika jamii.

Lugha hutumiwa kama nyenzo katika shughuli za ujenzi wa himaya. Kwa mfano, lugha ya Kilatini ilikuwa na jukumu kubwa katika uimarikaji wa himaya ya Warumi. Pia Warusi walipowafunza Kirusi kwa lazima wakazi wa Uropa ya Mashariki (hasa katika maeneo ambayo lugha hii haikuwa ikitumika) chini ya sera yao ya <u>Russification Policy</u> iliyoongozwa na viongozi wao walioitwa Tsar, shughuli yao ya kuitawala sehemu hii ya Uropa ilifaulu. Ni kwa sababu hii ndipo Joseph Stalin, katika kuthibitisha umuhimu wa lugha katika ujenzi wa himaya ya kilimwengu, alisema kuwa himaya za Cyrus the Great, Alexander the Great, na Charles the Great, hazikudumu kwa sababu kila moja ya himaya

hizi ilikosa kuwa na lugha moja ambayo ingeiunganisha pamoja (Goodman, 1977).

Ujuzi wa lugha fulani ni kama pasi ya kuingilia siasani katika jamii. katika nchi zilizogawika kimakabila kama vile Kenya na Nigeria ni nadra sana kumpata mtu asiyeongea lugha moja na walio wengi akipigiwa kura aende bunge kuwawakilisha. Pia katika nchi kama hizi watu hawana budi kuipita mitihani ya lugha ili kuruhusiwa kupigania viti. Nchini Nigeria kwa mfano, mtu hawezi kukubalika kuingia bunge kama hana ujuzi wa lugha ya Kiingereza. Katika hali kama hii, watu wasio na ujuzi wa Kiingereza wanaweza tu kupiga kura; na kwa hivyo ukosekano wa ujuzi wa lugha (ya Kiingereza) kwao huwafanya wawe ni watu wa kuitii sheria na wala si wa kushiriki katika kuitunga. Kwa hivyo lugha yaweza kumfanya mwanajamii akose maslahi ya kijamii yanayoenda na siasa.

Westermann, D (1934) yuasema kuwa hapana kitu kiwezacho kuwaleta watu pamoja kama ilivyo lugha moja. Anasema kuwa ni kwa sababu hii ndipo kote ulimwenguni utakuta kuwa kuna maeneo mijini ambapo wageni wanaozungumza lugha moja hukusanyika ili kupata kujikumbusha nyumbani. Pia si ajabu kupata watu kama hawa wakiwa wananunua majarida yaliyoandikwa katika lugha yao kwa sababu lugha ni kiungo muhimu kati ya waliko (ugenini) na nyumbani.

Hii ndiyo maana ya kuikazania lugha yao ugenini ili hisia na thamani za nafsini zipate kuhisika. Na mtu ye yote ambaye (katika mazingira ya ugenini) hukataa kuzungumza lugha yake ya asili hujitenga na watu wake.

Yaani lugha yaweza kuangaliwa pia kama chombo kibebacho tabia za watu. Mtu anapojitenga na wenzake kilugha, huwa amekosa kuingiliana na matakwa ya wanajamii na kwa hivyo anaweza kulaaniwa kama ambaye ana tabia tofauti na zile zinazotarajiwa. Pia, ikiwa watu watajifunza lugha fulani, tabia zinazoenda na hiyo lugha zitawalanda wao pia. Tuchukue kwa mfano tabia hii ya waswahili ya kuwa ni wajanja wajanja. Walipotuama Mumias waliwafunza wenyeji wa mji huu lugha yao na katika kufanya hili ile tabia ya Waswahili ya kuwa wajanja iliwaingia na kuwakolea watu wa Mumias. Kwa sababu hii, watu waishio Magharibi mwa Kenya wanawaogopa Waswahili na wao humwona mtu ye yote aliye mjanja kuwa ni Mswahili. Si ajabu kumpata mgeni anayekizungumza Kiswahili kwa ufasaha akishukiwa kuwa si mtu mzuri katika pande hizo za nchi ya Kenya. Tunachokisema hapa ni kwamba lugha yaweza kubeba tabia za watu katika jamii fulani.

Lugha pia hutumiwa kama dawa (kwa shibe) ya kisaikolojia. Mtu anapopata umilisi katika lugha fulani katika katika baadhi ya jamii, yeye huchukuliwa

kama mtu mwenye hadhi kuwazidi wale wengine katika jamii inayohusika. Kwa sababu hii utapata kuwa watu wanafanya juu chini ili wapate kujua baadhi ya lugha na kuzizungumza kwa ufasaha mkubwa. Kutokana na umuhimu unaopewa baadhi ya lugha, utapata kuwa watu watataka kuzitazama kama zilizo tukufu na ambazo huwahudumia wachache wateule katika jamii zinazohusika. Ni kutokana na hoja hii ya kisaikolojia ndipo baadhi ya watu huamini (au hufikiri) kuwa ni baadhi tu ya lugha ambazo zinaweza kutumiwa kama vifaa vya kutawalia watu na kuwa kamwe lugha zile nyingine haziwezi kulitekeleza hili. Pia ni kwa sababu hii ambapo utakuta watu wakijaribu kulinganisha uwezo wa mtu wa kuiongea lugha fulani na kiwango chake cha elimu. Yote haya ni mambo ya kisaikolojia.

Hapa lugha inajitokeza kama suala la kifikira. Lakini kuna na zaidi ya hili. Kwa kuwa lugha hiziathiri fikira za watu yaweza kuelezwa kama chombo kilicho na msingi katika asasi za kijamii na ambacho hutumiwa kuhifadhia historia na utamaduni wa jamii inayohusika.

## 2.3 Hitimisho

Utafiti kuhusu utendaji kazi wa lugha katika jamii uliofanywa katika sura hii umebainisha kuwa kule kuijua lugha fulani na kuweza kuitumia katika nyanda mbalimbali ya kimaisha huambatana na mambo mengine mengi yaliyo na misingi katika mahusiano ya

kijamii ya wazungumzaji. Ule utendaji kazi wa lugha ambao wajulikana na wengi - mawasiliano - hauwezi kusemekana kuwa unabeba yote ambayo lugha hufanya. Ikizidi, kwa mujibu wa maelezo kuhusu kazi ya lugha katika jamii hapo juu, inaweza kusemekana kuwa si lugha zote ambazo hukusudiwa mawasiliano tukichukulia mawasiliano kwa maana ya ile hali ya kuweza kubadilishana mawazo kwa matumizi ya maneno kama malighafi ya lugha. Lugha, kila mara, hufungamanishwa na mahusiano yaliyoko katika jamii. Kama asasi yo yote ile ya kijamii lugha huhitaji kuwaziwa kwa tuo na makini makubwa ili kupata kusema inatumiwa kwa maana gani.

Ni kwa sababu hii ndipo katika sura zifuatazo tutajishughulisha na maana ya kila tendo lililo-fungamana na maamuzi yo yote yale kuhusiana na lugha nchini Kenya. Kote swali linalotuongoza ni: Ni vipi ambavyo huu utendaji kazi wa lugha umeathiri maendeleo na kuimarika kwa Kiswahili nchini Kenya?

## 2.4 Tanbihi

1. Nukuu hii tumelipata kutoka kwa Utangulizi wa Dutton, T.E. (1976) katika mhadhara wake ambao aliuita Language and National Development; Long Wanem Rot ? - Chuo Kikuu cha Papua New Guinea.

2. Haya ni maneno ya Haugen (1966) akimunukuu Leach, E.R. (1954).

3. Rejelea Osundare, N (1981:99)

4. Soma aya ya pili ya ukurasa wa 18 katika <u>Bottlenecks to national Identity</u>: <u>Ethinic Cooperation Towards National Building</u>, kitabu kilichohaririwa na Ongong'a J.J na Gray, K. R.

SURA YA TATU

## 3.0 HALI YA LUGHA KATIKA KENYA YA KIKOLONI

### 3.1 Utangulizi

Akimnukuu Friere (1975:245) T.E. Dutton (1976:30) anasema kuwa kila mara elimu ni tukio la kisiasa na matukio ya kisiasa hayaji yenyewe bali husukumizwa baada ya mtu kufanya kitu fulani. Kwa kukumbuka hili, tunachambua hali ya lugha nchini Kenya katika enzi ya wakoloni wa Kiingereza kwa kuzingatia hasa nafasi zilizopewa Kiingereza na Kiswahili katika uwanja wa elimu na katika nyanja nyingine.

Sura hii inajaribu kujibu maswali kama haya yafuatayo: Wakoloni wa Kiingereza walipokuja Kenya walikuwa na sera gani ya lugha? Vigezo vilivyowaongoza katika uchaguzi wao wa lugha za kutumika katika mianda mbali-mbali, hususan wa elimu, vilijikita katika mantiki gani? Je, uchaguzi wa lugha kama huu ulikiwa na maana na makusudio gani?

Ni fikira yetu kwamba endapo tutachambua utendaji kazi wa Kiswahili, Kiingereza, na lugha nyingine za asili nchini Kenya tutachangia vikubwa mjadala kuhusu lugha nchini Kenya. Tunaanza kwa kueleza sera ya lugha nchini Kenya na sababu za kutokuwa na sera ya lugha isiyo wazi. Katika kufanya haya tutaendeleza pia maana

ya kila tendo linalofungamana na maamuzi yo yote kuhusu lugha. Katika kufanya hivi, tutaeleza athari za mahusiano ya kilugha ya aina hiyo katika jamii ya Wakenya ya wakati huo.

## 3.2 Sera ya Lugha Nchini Kenya Enzi ya Waingereza

Suala la sera halitekelezi holela bali huwa na mpango wake. Dhana ya mpango ina maana ya kufanya uteuzi kiurazini ili kuchagua njia mwafaka, miongoni mwa njia mbalimbali, na kuitumia kutatulia tatizo. Katika uchaguzi ufanywao, kunakuwa na kutiliwa maanani kwa athari zitakazojitokeza kutokamana na uchaguzi huo.

Katika upangaji wa sera ya lugha nchini Kenya wakoloni walikabiliwa na tatizo la lugha ipi itumike wapi, lini, na kwa matokeo gani. Basi katika sehemu hii tunajishughulisha na suala hili lugha nchini Kenya wakati wa ukoloni wa Mwingereza. Ingawa harakati za kuiendeleza lugha fulani, mahali fulani, kwa kuipa msukumo ni za kihistoria, hapa hatuielezi historia ya lugha nchini Kenya maana hili limekwisha kuelezwa kwingi[1] Tunaeleza namna hizo harakati zilivyojitokeza na kuendelezwa. Kimsingi, tunatoa fasiri za matukio na maamuzi mbalimbali kuhusu lugha kwa kujibu maswali: Kwa nini na kwa athari gani, bila kujiingiza sana katika maswala ya lini na wapi yalitukia.

Kiswahili ni lugha ambayo matumizi yake yalikuwa yameenea kwingi nchini Kenya hata kabla ya kuja kwa wakoloni wa Kiingereza. Je, hii ndiyo sababu ya pekee iliyowafanya Waingereza hawa kuitia maanani lugha hii katika utekelezaji wa sera zao za kikoloni? Lugha hii ilipewa jukumu gani kimawasiliano? Na jukumu hili liliathirije lugha hii katika kuimarika kwake?

Kulikuwa na makundi matatu makuu ya wageni nchini Kenya: Wamisheni, walowezi, na maafisa waliotawala kwa niaba ya serikali ya Uingereza. Watu hawa ndio waliokuwa katika pote la wageni wa kikoloni waliokuja nchini Kenya na ambao waliiathiri vikubwa hali ya lugha nchini Kenya. Hata hivyo, lazima tukumbuke kuwa wakoloni hawa hapa na pale walihitilafiana katika waliyoyasema kuhusu lugha. Wamisheni kwa mfano, wakiwa na lengo kuu la kufunza dini walitaka lugha itumike kwa kuwatekelezea jambo hili; nao masetla, kwa kuwa nia yao ilikukwa ni kutuama katika Kenya na kujiendeshea shughuli zao za kilimo bila kutatizwa walikuwa radhi kufanya lo lote lile ilmuradi Mwafrika akubali mahali pake katika jamii hiyo bila kusababisha vurugu na fujo. Kwa sababu hii, maoni ya walowezi hawa kuhusu lugha yaliwasawiri kama watu ambao daima walitaka kumwona Mwafrika na Uafrika kama vitu duni na ambavyo havikuhitaji makini yo yote.

Kundi la maafisa wa kikoloni nalo, kwa kuwa lilikuwa likitawala kwa niaba ya serikali ya Uingereza, lilikuwa radhi kutenda lo lote bora tu liwe limepewa maamrisho na idhini na serikali ya Uingereza. Miongoni mwa kazi muhimu ya watawala hawa ilikuwa ni kuwapa Waafrika elimu ya kuwawezesha kusaidia katika shughuli za kuimarisha utawala wa Waingereza. Lakini kutokana na umuhimu wa lugha maishani, haja ya kuwa na mpango fulani kuhusu lugha ilijitokeza kama jambo muhimu na la lazima. Kwa kutambua umuhimu wa mashule katika kuendeleza na kuimarisha lugha, watawala, wakishirikiana na wamisheni walianzisha mashule katika koloni ya Kenya. Mifumo ya mashule iliyoanzi~~wa~~shwa iliingiliwa hapa na pale na serikali ya kikoloni maana ilitaka kuathiri lugha ambayo kwayo Waafrika walifunziwa. Hii ilikuwa hivi kwa sababu

> Ni jambo linalofahamika kuwa lugha na siasa ni mambo mawili yanayoingiliana katika jamii za ~~ki~~siku hizi. Kile ambacho mtu huwa, wapi na lini hutegemea lugha anayoizungumza na asiyoizungumza. Na hili huwa ni suala lenye utata zaidi mtu anapokuwa katika taifa lenye lugha nyingi.
>
> (Mutahi, K. E. 1980:1)
>
> (Tafsiri Yetu)

Yaani, mifumo ya mashule ambayo Waingereza walikuwa nayo nchini Kenya ilikuwa ni sehemu tu ya sera ya

Kikoloni ambayo Waingereza walikuwa nayo, na iliyojengeka katika njia ya utawala isiyo ya moja kwa moja iitwayo Indirect Rule.

Kati ya makundi ya wageni waliokuwa katika koloni ya Kenya, ni kundi la masetla lililokuwa na sauti zaidi ya yote katika masiala yaliyohusu koloni hilo. Sababu ya tapo hili kuwa na nguvu ni kuwa ndilo lililotegemewa na serikali ya Uingereza katika mazao, malighafi mabalimbali, na katika shughuli nyingine za kiuchumi. Na hapa hatuna budi kukumbuka kuwa lengo kuu la kuanzisha makoloni kote ulimwenguni lilikuwa na misingi katika ubepari. Ni hali hii ya 'mwenye nguvu' na 'ase nguvu' za kiuchumi ambapo lugha ya Kiingereza, Kiswahili, na za asili zilitegemea maana ndiyo iliyoipa sera uzima ya lugha nchini Kenya msukumo na mwelekeo.

Kwa kufuata sera yao ya kikoloni, Waingereza katika koloni yao ya Kenya mara wangefundisha na kuhimiza matumizi ya kiingereza, mara ya Kiswahili, na mara lugha nyingine za asili. Hii sera ilikuwa na malengo fulani.

Kijumla, wakati huu, thamani iliyopewa Kiingereza, Kiswahili, na lugha nyingine za asili nchini Kenya ilikuwa na umuhimu katika mpango wa sera ya lugha iliyokuwa katika koloni ya Kenya. Wakati huu, baadhi

ya wamisheni walikataa kukitumia na kukiendeleza Kiswahili kutokana na mafungamano yake na Uislamu. Dini ya Kiislamu imekuwa ni dini pinzani kwa Ukristo na kwa hivyo kwa kuhujumu matumizi ya Kiswahili, wamisheni walitegemea kuififisha dini hii vile vile maana ilitumia Kiswahili katika mahubiri yake. Wakati huo huo, serikali nayo ilikuwa na sera iliyopigania utengano nchini. Sera hii ilijitokeza hata katika kipengele cha lugha.

Wakoloni walijua kwamba kuwa na lugha moja nchini Kenya kungesaidia katika kuleta umoja nchini. Umoja wa aina hii ungehasiri na kuhatarisha kuwa kwao nchini Kenya maana hapangekuwa na kule kupashana 'siri' miongoni mwa watawala na zisiweze kufahamika na umma wa watawaliwa. Kwa sababu hii, wakoloni hawa, katika upangaji wao wa sera ya lugha, walizifikiria pingamizi ambazo zingezushwa na wananchi wa Kenya kufungamana na sera yo yote ile ya lugha ambayo wangekuwa nayo. Yaani sera ya wakoloni kuhusu lugha nchini Kenya ilipangwa kwa njia ambayo kwamba ingewafaidi wakoloni hawa. Lakini walihitaji waendelezaji wa sera hii, ambao wangekuwa pamoja na Waafrika.

Ili kuwafanya Wakenya wasaidie katika shughuli hii, wakoloni walibuni vivutio vilivyojengeka katika asasi za kiuchumi na kijamii nchini Kenya. Hii sera ililenga katika kuwa na makundi mbalimbali yakijitambulisha na kujitofautisha na mengine. Wakoloni walioona hali hii kama iliyo mwafaka zaidi maana ingezalisha hali ya mtafaruku miongoni mwa Wakenya wenyewe kwa wenyewe na hivyo kuwarahisishia wakoloni kazi yao ya kutawala dhidi yao (Wakenya).

Kwa kuwa elimu ni muhimu katika utekelezaji wa masuala ya sera ya lugha, wakoloni walijitokeza na mpango madhubuti wa elimu uliofungamanishwa na maendeleo ya watu kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ni kwa sababu hii ndipo inakuwa muhimu kukumbuka matukio muhimu ya kilugha na kiutamaduni pamoja na yale ya kisiasa yaliyowahi kutukia nchini Kenya ili kuelewa vyema sera ya lugha nchini Kenya. Kimatumizi, kulikuwa na mpaka kati ya Kiingereza na Kiswahili. Mpaka huu ulikuwako kwa sababu za kisiasa na matakwa ya kiuchumi yaliyokuwa yamesimikwa na wakoloni. Kadri ulivyopita muda, Kiingereza na Kiswahili, pamoja na lugha za asili, kila mojawapo ilipewa majukumu yake, mbali na kuwa vyombo vya mawasiliano. Kiingereza kilitumika kama lugha ya

kutawalia katika ngazi za juu huku Kiswahili kikitumika kama lugha iliyowaunganisha wafanyakazi katika mashamba ya Wazungu au katika huduma nyingenezo za serikali ya kikoloni. Lugha za kienyeji nazo zilitumika katika mawasiliano ya ndani kwa ndani miongoni mwa watu wa kabila moja. Pia hapa na pale wamisheni wangezitumia katika kuhubiria dini maana waliamini kuwa ndizo zilizofaa zaidi kwa shughuli hii. Hali hii ilikuwa na maana fiche.

Wamisheni, wafanyakazi wa kikoloni,na maajenti wa serikali walikitazama Kiswahili kama njia ya kuufuta mpaka uliokuwako kati ya watu wa makabila mbalimbali. Katika hali kama hii, wamisheni walipigania uendelezaji wa Kiswahili kwa sababu kulikuwa na haja ya kuwa na lugha moja ambayo ingetumika katika shughuli za kielimu na za kidini kote nchini.[2] Ni Kiswahili ambacho kingefaa zaidi kulitekeleza jukumu hili kwa sababu hata kabla ya ukoloni wa Mzungu lugha hii ilikuwa imeenea na kushika kwingi. Basi, hawakuona ni kwa nini isitumike sasa ambapo harakati nyingi za matumizi yake, zikiwemo za kielimu, zilikuwa zikitekelezwa.

Mtazamo huu ulikinzana na ule wa wakoloni. Katika kupata wafanyakazi wa Kiafrika ambao wangesaidia katika uendelezaji wa kazi zao za kiutawala na kazi



UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

nyingine kama vile kufunza, kuwa makarani, matarishi, n,k, serikali ya kikoloni haikukithamini sana Kiswahili. Mbali na kuwa ujuzi wa Kiingereza ungempa mtu kazi nzuri na yenye mshahara mkubwa, sera yao ya uajiri iliwapendelea Wakamba kama askari-jeshi, Wajaluo kama polisi na Wabaluhya kama wapishi na mashamba-boi[3]. Waswahili nao hawakuwa na kazi yo yote ambayo ingeweza kusemekana kuwa ilikuwa yao. Hali kama hii haingeweza kufanya lugha yao - Kiswahili - iendelezwe vyema.

Sababu nyingine ambayo ilikififisha Kiswahili katika kuendelea kwake ni hali ya wamisheni ya kupigania ufunzaji wa lugha za asili katika madarasa ya chini ya shuleni. Tukijua kwamba ni katika madarasa haya ambapo misingi ya masomo mbalimbali huwekwa, hali hii ilikuwa na athari kwa kuimarika kwa Kiswahili[4]. Bila shaka hali hii ilitokea kwa sababu ya athari za serikali ya kikoloni kwa wamisheni.

Mpaka hapa suala kuu ni mtazamo wa wakoloni hawa dhidi ya aina hii ya sera ya lugha. Wakati huu Kiingereza ndicho kilichokuwa lugha rasmi. Ni katika uwanja wa elimu kulikokuwa na matatizo. Ili elimu iweze kusaidia katika harakati za 'mapinduzi' katika koloni la Kenya, lugha ambayo kwayo masomo yaliendeshwa iliweza kutawaliwa nao pia. Hii ni ithibati-tosha kuwa msukumo wa aina hii ulitokana na serikali-mzazi kwa koloni ya Kenya. Haikosi

hali hii ilitokana na sababu kuwa wao (Waingereza) walitaka utamaduni wao umwingie na kumkolea Mwafrika. Hali hii pia ingeweza kumulika na kutathmini mahusiano ya watu nchini Kenya na kuweza kusema ikiwa Waingereza wamefaulu au la. Ilihofiwa kuwa matumizi mengi ya Kiswahili yangewahasiri baadhi ya Wazungu ambao hawakuthibiti matumizi yake katika kuwasiliana na Wakenya. Wakoloni walikuwa wamekuja, miongoni mwa mengine, kufanya biashara na kujitajirisha kadiri ya uwezo wao. Basi wao waliona kule kufanywa kwa Kiswahili kuwa lingua franka nchini Kenya kama tisho kwa biashara yao maana katika hali hii, ni wale wenye uthibiti wa Kiswahili tu ambao wangethaminiwa kibiashara. Wenye ujuzi wa Kiingereza wangeambulia patupu.

Suala hili la lugha nchini Kenya ni telezi, tena tata. Je, katika kuwafunza Wakenya Kiingereza na kukipa umuhimu wote kilichopewa hiki ndicho kitu muhimu zaidi walichokihitaji Wakenya wakati huo? Kufunzwa kwa Kiswahili, Kiingereza, na lugha nyingine za asili huku kila mojawapo ikipewa umuhimu tofauti na nyingine kulifanywa kimakusudi kufungamana na matakwa ya sera nzima ya wakoloni wa Kiingereza nchini Kenya. Kama Kiingereza pekee kingesisitizwa, hali hii ingewafanya Waingereza nchini Kenya kutojishughulisha na kujifunza lugha za Kikenya.

Hivi ingekuwa vigumu sana kwao kuzielewa siri za Wakenya. Ili kuwaelewa Wakenya iliwalazimu wakoloni hawa kuwa na ujuzi wa Kiswahili pia. Ingekuwa kazi ngumu sana kwa wakoloni kuwatawala kama hawakufahamu lingua franka yao - Kiswahili - pamoja na lugha nyingine za asili.

Wakati huo huo pia, wakoloni walijua kuwa kufunza Kiswahili ambacho kilikuwa lingua franka nchini Kenya kungesaidia Wakenya katika kuungana kwao. Pia, walijua kuwa hali hii ingefikiwa, japo baada ya muda mrefu, ikiwa wangewahamasisha Wakenya kujifunza Kiingereza badala ya Kiswahili. Kwa hivyo walifunza Kiingereza - hasa katika daraja za juu za elimu - maana waliamini kuwa walikuwa na jukumu kubwa la kuwapa Wakenya ustaarabu.[5] Nao waliamini kuwa ustaarabu ulipaswa kumwingia Mkenya kupitia kwa Waingereza kama wendakati. Lakini Waingereza wawa hawa hawangeweza kukifunza Kiingereza kidhati maana hili lingekuwa kosa maana Wakenya wangeweza kuyafikia maandishi ya kimapinduzi ambayo yalipaswa kufichwa.[6] Mbali na kuwa maandishi haya yangezivuruga fikira za Wakenya, pia yangewatayarisha Wakenya kwa mapinduzi ambayo yangewafukuza Wazungu.

Nchini Kenya basi, hakukuwa na lugha moja ya matumizi. Kiingereza, Kiswahili, na lugha nyingine za asili zilitumika. Tunaweza kuamini kuwa kulikuwa

na juhudi za kimakusudi zilizofanywa ili kutokipa Kiswahili umuhimu ambao kilistahili kama lingua franka nchini Kenya na katika Afrika ya Mashariki na ya Kati kwa jumla. Katika kipindi kizima cha ukoloni, hapana po pote ambapo Kiswahili kilisisitizwa kama lugha ya pekee ya Kiafrika nchini Kenya. Hata baadhi ya wamisheni walikipuuza na badala yake wakasisitiza lugha nyingine za asili nchini Kenya pamoja na Kiingereza. Wao hawakujali sana suala hili la lugha. Badala yake walijishughulisha na kazi yao ya umisheni ambayo ililenga katika kuzalisha walimu wa dini na uendelezaji wa dini ya kikiristo kwa jumla. Kwao, lugha ya asili ilifaa maana ingerahisisha kazi yao. Hii ina maana kwamba Wamisheni wengi hawakuwa hasa maajenti wa elimu katika koloni la Kenya. Huku kusisitiza lugha za asili badala ya Kiingereza, hata hivyo, kulikuwa na athari ya kupunguza uwezekano wa kuwa na wataalamu wa Kiafrika maana wakati huo ni Kiingereza kilichokuwa lugha ya taaluma mbalimbali nchini Kenya. Na hili lilifanywa kimakusudi maana Wazungu wengi hawakutaka kuwe na Waaafrika ambao wangezielewa siri zao kupitia lugha zilimokuwa.

Yaani elimu iliyopewa Wakenya ilienda sambamba na matakwa na maslahi ya kiuchumi ambayo Waingereza wangepata. Kwa kuwa chaguzi za lugha za kutumika mahali fulani, mara nyingi, hutegemea lengo la

wachaguzi, lugha za asili pekee hazingeweza kutumika katika shughuli za elimu kwa kuwa Waingereza hawakutaka Wakenya wakae tu vijijini mwao; waliwataka wasaidie katika harakati zao za kujiendeleza kiuchumi kwa kutoa huduma rahisi. Kwa upande mwingine, kufunza Kiswahili kungewafanya wenyeji wawaone Waingereza kama watu ambao hawangeweza kuwalazimishia watawaliwa lugha yao. Hali hii ni ya kisiasa maana lugha ni nyenzo mojawapo ya kukita ukoloni. Kuwalazimishia watawaliwa lugha ya watawala kuna maana ya kuwatawala kilugha pia. Ni kwa sababu hii ndipo Kiingereza kikapewa umuhimu mkubwa kama lugha ya masomo ya juu na ya taaluma za kiteknolojia. Ilibidi Kiswahili nacho kifunzwe ili kiwe ni kiunganishi cha watu wote nchini Kenya kutokana na hali yake ya kusambaa kote nchini Kenya.

Ni katika misingi hii ndipo Kiswahili kikawa na hadhi ambayo kilipewa na Waingereza walipokuwa wakoloni nchini Kenya. Ni hadhi hii iliyokipa Kiswahili nafasi ya maendeleo yake. Kwa kuwa wakoloni walihisi kuwa ilikuwa hatari kwa watu wote - watawala na watawaliwa - kupewa haki sawa, walijitahidi kutozalisha hali hii kilugha. Na kwa kuwa elimu ni mbinu muhimu sana katika kuzalisha hali ya kuziathiri na kuzikengeusha fikira za watu, wakoloni waliamua kuwa na sera ya elimu na ya lugha tuliyoitaja hapo juu ambapo Kiingereza kilikubaliwa na Wakenya wenye kisomo

kama lugha tukufu.

Basi kulikosa kuwa na muala wa kilugha nchini Kenya. Kulizuka hali ya kuwa na matumizi ya lugha kijamii ambapo mafalahi, wakulima vijijini, na wafanyakazi wa viwango vya chini walitengwa na wenzao wenye kisomo cha juu na ambao kazi zao zilikuwa na mishahara mikubwa-mikubwa. Basi tofauti za lugha, mbali na kuwa zilisababisha utengano kimawasiliano, pia ziliwafanya baadhi ya Wakenya kukubalika au (na) kutokukubalika katika nyanja mbalimbali za kijamii. Wale Wakenya waliokosa kukimudu kiingereza walitazamwa kama walio duni kiutamaduni na wasiostaarabika; na kutostaarabika kulimaanisha kuwa duni kiuchumi.[7] Kwa upande mwingine, ujuzi wa Kingereza ulimaanisha nguvu za kisiasa na zile za kijamii ambazo zilishirikiana kumpa mtu uwezo wa kuhodhi mali mengi. Basi, kwa Wakenya, ujuzi wa Kiingereza ulikuwa ni kitegauchumi maana ulitumika kama kivutio uchumini. Na kwa kufaulisha hili, serikali ilijitokeza na sera ya lugha tuliyoizungumzia katika kijisehemu hiki.

## 3.3 Tathmini ya Hali ya Lugha Kenya Nyakati za Ukoloni

Hakukuwa na sera wazi ya lugha nchini Kenya nyakati za enzi ya wakoloni wa Kiingereza kwa kuwa katika katiba ya koloni hii hakukuwa na maandishi yo yote ya kisheria ambayo yalisema lugha fulani ingekuwa na kazi hii nayo fulani iwe na hii. Lakini kutokana na hali ya lugha nchini Kenya, kama tulivyoieleza, ilichukuliwa kuwa Kiingereza kilikuwa ni lugha yenye hadhi na ambayo ilifaa kutumika katika shughuli za kitaifa kuliko lugha zote nchini Kenya. Ni kwa sababu hii ndipo Kiingereza kilifanya kazi kama lugha ya Taifa, na ndiyo iliyokuwa lugha ya kufundishia katika viwango vya juu vya elimu, ya kufanyia biashara ya kitaifa na kimataifa, na ndiyo iliyotumika katika utawala wa daraja za juu. Katika kutimiza majukumu haya makubwa, Kiingereza kingesaidiwa hapa na pale na Kiswahili pamoja pamoja na lugha nyingine za asili ingawa lugha hizi zilitengewa kazi maalumu. Lugha za asili zilitumika katika mawasiliano ya kikabila. Kiswahili nacho kilitumika katika kusahilisha mawasiliano baina ya watu wa makabila mbalimbali au katika ngazi za chini za utawala.

Kwa kuzitengea lugha za asili na Kiswahili nyanja hizi za matumizi, Waingereza walikuwa wamezidharau lugha hizi. Kiswahili, kwa mfano, kilisemekana kuwa ni lugha isiyo na wenyewe. Hali hii ilizidishwa na kule

kutopewa nafasi kwa lugha hizi katika ngazi za juu za elimu, kama lugha ya Kiingereza ilivyokuwa. Kwa sababu hii, mtu alihesabika kuwa ameelimika tu pale alipoweza kukizungumza Kiingereza kwa ufasaha mkubwa. Mtu asingeweza kutazamwa hivi kutokana na ujuzi wake wa Kiswahili.

Hali hii ilizalisha machukulio ambayo mihimili yake ilikuwa katika mielekeo ya maendeleo waliyoyataka wakoloni wa Kiingereza. Baadhi ya machukulio haya yalijitokeza katika aina za elimu zilizokuwako ilhali mengine yalikuwa na misingi katika hali ya kijamii ya Wakenya wakati huo. Ni kutokana na umuhimu wa lugha katika elimu na maisha kwa jumla ndipo H.C. Helman (katika Fishman, J.A. 1972:211) anasema kuwa sera yo yote ile ya lugha iliyoundwa huenda isifaulu kama haikushirikiana na mpango wa elimu pamoja na maendeleo ya kiuchumi na kisiasa.

Basi Kiingereza kilisisitizwa kwa sababu Waingereza walitaka kuitumia lugha hii ili kuunda himaya moja kubwa ulimwenguni. Kiingereza kingeiunganisha Kenya na koloni nyingine za Uingereza. Lakini lugha hii ya Kiingereza haingeweza kufunzwa kiholela maana ilikusudiwa madhumuni maalum ambayo yalikuwa, miongoni mwa mengine, kuifanya sehemu fulani ya umma wa Kenya kujihisi kuwa ni tofauti na sehemu nyingine na wakati

huo huo kujifananisha na umma mkubwa wa wazungumzaji wa Kiingereza. Ni katika hatua hii ndipo suala la ni lini, na vipi Kiingereza kianze kufunzwa wenyeji likazuka.

Na ili lugha yo yote ile kupata kutumika kwa makusudio fulani ya kijamii, haina budi kujulikana vyema zaidi ili wazungumzaji wake wapate kuielewa katika viwango vya juu. Ujuzi wa aina hii kuhusiana na lugha huchukua muda mwingi sana wa masomo kuweza kupatikana. Wakenya walianza kufunzwa Kiingereza walipofika madarasa ya kati ya shule za msingi. Na ili kuingia katika madarasa ya juu ya shule za msingi, walifanya mitihani ambayo iliwachuja na kuwaacha wachache tu waendelee na masomo. Katika hali kama hii, ni Wakenya wachache sana waliopewa misingi imara ya Kiingereza. Hawa ndio ambao baadaye walipewa kazi za utarishi, ukarani, ualimu, n.k.

Kwa sababu ya hali ya kisomo chao, walijihisi kuwa ni watu bora kuliko wale wengine ambao hawakusoma Kiingereza kufikia viwango kama vyao. Hali hii ilisababishwa na kule kufunzwa kwa Waafrika Kiingereza maana kama anavyosema H.C. Kelman (Katika Fishman, J.A. uk 209)

> Lugha yaweza kusaidia kufufua na kuongeza hali ya muda mrefu ya kutoelewana kati ya

> makundi. Tatizo hili laweza kuongezwa na ile hali ya watu muhimu katika kundi tegemezi, ambalo lafahamu lugha muhimu, kujiboreshea hali za maisha yao huku likikengeuka kutoka kundi lao.
>
> (Tafsiri Yetu)

Ingawa kundi hili la Wakenya lilijihisi hivi, halingeweza kukubalika katika kundi la Waingereza (na Wazungu wengine) kwa sababu ya rangi ya ngozi zao. Basi kulitokea kuwa na makundi matatu nchini Kenya na ambayo yalijengeka katika msingi wa lugha. Hawa walikuwa ni Waingereza (na wazungu wengine), Waafrika wenye kisomo chenye misingi katika ujuzi wa Kiingereza, na Waafrika waliokifahamu Kiswahili (kwa sababu ya kuwa kwake lingua franka) na lugha za asili.[8]

Kiingereza kilikusudiwa kuwapumbaza wakenya ili wasaidie katika kuwazalishia wakoloni malighafi rahisi na huduma nyingine ambazo zingewaendeleza kiuchumi. Basi kule kuwapa Wakenya elimu kupitia Kiingereza ilikuwa ni mbinu ambayo kwayo uchumi wenye misingi ya Kimagharibi ungekitwa nchini Kenya. Kwa sababu hii, mahusiano ya kiuchumi kati ya Kenya na mataifa ya kimagharibi yangekuwa kwamba daima Kenya ingetegemea mataifa haya kujiendeleza

kiuchumi. Ilikuwa katika kuhakikisha kwamba hili liliendeshwa bila pingamizi ndipo lugha ya Kiingereza ikawa ni hifadhi ya wachache waliochunjwa kutoka kwa umma mkubwa wa Wakenya. Wakati huo, kufeli Kiingereza katika mitihani kuliweza kuathiri vikubwa sana thamani ya cheti alichokipata mtu. Hali hii ingemfanya mtu akose kazi serikalini. Basi ni Wakenya wachache tu ambao walipewa elimu ya Kiingereza na wakaitumia katika shughuli zao za ujenzi wa koloni hilo. Bila shaka Waingereza walitaka hali iwe hivi ili waweze 'kuwanunua kirahisi' wale Waafrika wachache kwa kuwafanya wahisi kwamba maslahi yao ni afadhali kuliko yale ya Wakenya wengine.

Ili kuwahamasisha waafrika katika hili, wakoloni walikuwa na mikakati iliyojengeka katika saikolojia. Waliwapumbaza Wakenya kwa kuwaeleza kuwa utamaduni wa Mwingereza ulikuwa bora na wa hali ya juu ukilinganishwa na ule wa Mwafrika katika vipengele vyake vyote. Hili lilikuwa na maana kuwa lau Wakenya wangejifunza Kiingereza, basi, kingewasaidia kujiinua angaa kwa kipengele hiki kimoja cha lugha. Hoja hii ni ya kitaasubi na ilipendekezwa na baadhi ya wanaanthropolojia ambao waliamini kuwa kuna tamaduni zilizoendelea na zile ambazo hazikuendelea. Kwa wanaathropolojia kama hawa, lilikuwa ni jukumu la watu wa tamaduni zilizoendelea kuwainua wale ambao tamaduni zao hazikuendelea.

Lakini Waingereza hawakufaulu kwa hili kwa sababu katika kuwafunza Wakenya Kiingereza walianzia katika kiwango cha juu cha elimu ya Wakenya hawa. Katika hali kama hii, Waingereza hawangeweza kuwanyofoa Wakenya kutoka katika Uafrika na kuwaelekeza Uzunguni. Ikizidi, kile walichokifanya ni kuwafanya Waafrika hawa waning'inie katika tamaduni mbili: wa Kiafrika na wa Kizungu. Hali hii iliwatia Wakenya walioelimika katika hali ya kiutumwa kiutamaduni na kilugha maana lugha ya Kiingereza iliathiri vikubwa maoni ya watu hawa kuhusu tamaduni zao.[9]

Yaani ile elimu waliyopewa Wakenya, na ambayo ilisisitiza sana Kiingereza, ilikusudiwa kuwagawanya katika matabaka ya kiutamaduni. Hali hii ndiyo iliyofanya baadhi ya watu wajihisi kuwa bora dhidi ya wengine. Hii ilikuwa ni mbinu ya kuwagonganisha Wakenya ili kuwatawala kirahisi kama ambavyo imefafanuliwa katika sera ya kikoloni ya Waingereza nchini Kenya. Wale waliokuwa na elimu ya Kiingereza walikuwa katika mkondo wa mabepari uchwara. Kwa sababu hii walifanya juu chini kupigania maslahi ya Wazungu maana walijua kuwa kuendelea kwao (wao) kuliwategemea Wazungu. Yaani, mfumo wa elimu uliokuwako nchini Kenya katika enzi ya wakoloni wa Kiingerreza uliwatayarisha

kuwa 'watumishi' wa wageni hawa. Ni katika hali hii ndipo Wakenya walipoteza (kwa dharau) Kiswahili ilhali hii ni lugha ambayo ingewatambulisha kama watu wa eneo moja kutokana na kule kuwa kwake lingua franka enzi hizo.

Lugha ni kifaa kiunganishacho watu wenye tajriba moja katika kundi. Hili lingefanywa na Kiswahili nchini Kenya lau kingepewa fursa ya kuendelea. Kwa kuchelea athari za kuendelea na kuimarika kwa Kiswahili Waingereza walikosa kukipa msukumo ambao kilistahili. Badala yake waliwapa Wakenya motisha ya kijifunza Kiingereza ili kuzivunja zile kasi ambazo Kiswahili kilikuwa nazo kuhusiana na kuwaunganisha watu. Basi Kiingereza kililetwa katika mfumo wa elimu na wa mawasiliano ili kuwa nyenzo ya kuleta mgogoro na kutoelewana pamoja na kutothaminiana miongoni mwa Wakenya. Ni hivyo ambavyo ule ujenzi wa taifa lisilo na misingi ya kiutamaduni ulishika kasi maana hakukuwa na kuheshimiana katika koloni hili la Kenya, mbali na kuwa lilipoteza utambulisho wake kama taifa lenye kuthamini mambo fulani mamoja mathalani lugha.

Katika wakati huu, Waingereza walikuwa wamejitokeza na mkakati wa kuthibiti kutoendelea kwa Kiswahili kwa kubana matumizi yake. Mkakati huu ulijikita katika ukweli kuwa wale watu waliokuwa na ujuzi

wa Kiingereza ndio waliopata kazi ambazo kwingine zilifanywa na Wazungu, na ambazo ziliwapa watu mali na hadhi pamoja na 'heshima' katika jamii. Kiswahili, kwa upande mwingine, kilitumiwa na watumishi, maboi, wanyapara, n.k. katika kuwasiliana na waajiri wao na ambao hawakujali sana kuhusu sarufi ya Kiswahili walichokizungumza.

Hizi zilikuwa ni juhudi za kimakusudi za kukiendeleza Kiingereza na kukidunisha Kiswahili. Lakini juhudi hizi hazingekuwa hivyo kama si kwa sababu nyingine muhimu ya kiuchumi. Mojawapo ya sababu kuu za makoloni kutafutwa ilikuwa ni ile ya kutafuta mawezekano ya kuwafanya baadhi ya wananchi (waliokuwa wengi zaidi kutokana na athari za Mapinduzi ya Viwandani) kutuama. Lakini kutuama tu hakungetosha. Walihitaji kujishughulisha na mambo mbalimbali ya kiuchumi maana msingi wa makoloni ulikuwa katika biashara. Basi Waingereza walikazania kufunza Kiingereza ili kuwapa kazi watu wa kwao ambao wangefunza Kiingereza na masomo mengine kwa kutumia Kiingereza. Hali hii ingeweza kuwaendeleza kiuchumi na kijamii. Katika hali kama hii, ule mwanya wa kijamii kati ya Wazungu na waafrika ungezidi kuwa mkubwa.

Hizi sukumizo za Kiingereza zilikusudiwa kuifanya lugha hii yenye umuhimu mkubwa zaidi ya zote nchini Kenya. Kwa kuwa lugha humulika utamaduni wa watu, kule

kukiimarisha Kiingereza kulikuwa na lengo la kuufanya utamaduni wa Wakenya uwe, kimsingi, ni wa Kimagharibi. Kwa kuwa utamaduni huu umejaa ubinafsi, hasa katika mifumo yake ya kiuchumi, uliwafanya Wakenya ambao Kiingereza kwao ilikuwa ni ndoto kuporomoka kwenye ngazi za kijamii maana hawangeweza kusaidiwa na wenzao. Kama Kiswahili kingepewa msukumo hali isingekuwa hivi maana kingewaunganisha watu wengi katika mawasiliano ya ndani kwa ndani nchini, ya kimasomo, na ya kiserikali na kiutawala. Pia ingetumika kukuzia utamaduni na utaifa wa Wakenya.

Basi Kiingereza kilifunzwa kama njia mojawapo ya kuwakengeusha Wakenya. Lakini katika kuwafunza Wakenya Kiingereza, wakoloni hawa waliona hatari ambayo ingejitokeza. Hali hii ingeweza kuinua kisomo cha Mwafrika na wakati huo huo kumfanya ayaone mambo ya kisiasa kiuyakinifu. Hali hii ingekuwa hatari sana kwa usalama wa koloni nzima maana ingedai uhuru. Ni kwa sababu hii ndipo kukawa na uchujaji mwingi masomoni ambapo ni wale waliofaulu mitihani pekee walioruhusiwa kuendelea na masomo. Bila kujiingiza katika masuala ya utungaji na usahihishaji wa mitihani hii, jambo la kukumbukwa ni kwamba, kwingi, Kiingereza kilichofunzwa Wakenya kilinuiwa kusaidia kuendeleza mfumo wa kikoloni bila kuuhatarisha.

## 3.4 Hitimisho

Suala la lugha nchini Kenya nyakati za ukoloni wa Mwingereza lilikuwa na misingi katika siasa na uchumi. Hali hii ndiyo inayodhihirishwa na aina ya elimu waliyoitoa Waingereza kama ambavyo imerekodiwa katika historia ya lugha nchini Kenya. Lugha za asili, kikiwemo Kiswahili, zilifunzwa katika madarasa ya chini huku Kiingereza kikifunzwa katika yale ya juu. Ni katika madarasa haya ya juu ambako watu walipata ujuzi wa kufanya kazi kama vile ukarani na kazi nyingine ndogo ndogo ambazo zingesaidia kurahisisha kazi ya Waingereza ya kutawala.

Hali ya kuwa Kenya ni nchi yenye wingi wa lugha iliwafanya Waingereza wabuni mbinu ya kuwateka bakunja na kuwatawala wazungumzaji wa lugha mbali-mbali kilugha. Kwao, ni umuhimu wa kila lugha uliofanya ipewe hadhi yake. Matumizi ya lugha za asili katika madarasa ya chini na kule kufuatilizwa na mchujo ambao ungeruhusu watu wachache tu kusonga mbele na kujifunza (na kusomea katika) Kiingereza yalikuwa ni maamuzi yaliyolengwa katika kuwanyima Wakenya nafasi za kufanya kazi zilizokuwa zikifanywa na Wazungu na ambazo mishahara yake ilikuwa mikubwa. Waingereza pia waliwanyima Wakenya Kiingereza chenye kina, maana walihofu kuwa hivi Waafrika wangeupata ujuzi wa kiteknolojia ambao wangeutumia ili kusababi-sha hali ya ushindani dhidi ya Waingereza katika kazi za aina hiyo. Pia Kiingereza kingewezesha Wakenya

kupata maandishi ya kimapinduzi na kubadilishana mawazo ya kimapinduzi - hali ambayo ingehasiri nafasi za wakoloni hao nchini Kenya. Si hayo tu; hali hii pia ingewafanya Waafrika wajilinganishe na Wazungu ki-ulama.

Uhimizaji wa Kiswahili nao uliwaogofya Waingereza maana ungewasawiri kama watu wasiothibiti matumizi yake, na hali hii ingewafanya wakose 'siri' za Wakenya. Hali hii iliwatia Waingereza katika kilinge kilugha. Hata hivyo, kama watawala, walijitokeza na sera ya kikoloni ambayo ilijaribu kuiendeleza Kenya kiuchumi lakini pia wakati huo huo ikaathiri kasi ya maendeleo yake kwa kuchelea kupoteza koloni hiyo yao.

Kama tulivyotaja kwingine, lugha ina uwezo wa kujitokeza kama nembo ya utambulisho. Kule kujivunia Kiingereza kwa Waingereza, hata pale hali hii ilipokuwa hatari kwao, kulikuwa ni sehemu ya fahari waliyouonea utamaduni wao. Ni kwa sababu hii ndipo wakaishikilia lugha hii hata nje ya nchi yao. Wakenya walipewa utamaduni huu kupitia kwa elimu waliyopewa. Lakini elimu ya juu waliyoipata Wakenya, kama vile Kenyatta, iliwafanya kudai uhuru. Je, uhuru huu ulikuwa ni uhuru kwa jina tu au uhuru kidhati? Hili ndilo suala kuu tutakalojishughulisha nalo katika sura ijayo kwa kuzingatia hoja kuwa lugha

fulani inaponyang'anywa jukumu la kuwa na matumizi katika elimu ya juu, sheria au serikali, hili linakuwa ni shambulio la jamii inayoongea lugha inayohusika katika vipengele vyake vyote. Ni shambulizi kama hizi ambazo hudhihirisha kuwa wazungumzaji wa lugha mbalimbali wamo katika matabaka mbalimbali ya kijamii.

## 3.5 Tanbihi

1. Historia ya Kiswahili imeelezwa kwingi sana. Whiteley, W.H.(1969) amelishughulikia suala hili kwa mapana. Pia Chiragdin, S na Mnyampala, M katika <u>Historia ya Kiswahili</u> wamelishughulikia.

2. Hoja hii yaelekea kukinzana na ile nyingine tuliyotoa mwanzo kuhusu wamisheni kukataa kukiendeleza Kiswahili kwa sababu ya mafungamano yake na uislamu. Ndivyo hali ilivyokuwa katika hatua zake za mwanzo lakini baadaye walilazimika kukikubali Kiswahili kutokana na kutangaa kwake kote nchini Kenya.

3. Ingawa inaweza kusemekana kuwa hoja hii haina ithibati-tosha, lazima tujue kwamba mambo yalivyo sasa yana msingi wake katika jana. Mbona wapishi wengi sana mjini Nairobi - hasa katika maeneo yaliyokuwa ya Wazungu kama vile Kileleshwa - ni Wabaluhya?

4. Kwa maelezo kuhusiana na umri ambao mtoto anayejifunza lugha ya pili atapata kuifahamu vizuri sana, rejelea Johnson, K (1975) na Niyekawa-Howard (1972:5). Kimsingi wanaeleza kuwa umri muhimu wa kujifunza lugha ya pili ni toka kuzaliwa kufikia umri wa miaka kumi.

5. Tumetumia meno 'ustaarabu' hapa kwa maana ya civilization. Kwa sababu ya taasubi zao, Waingereza waliamini kuwa ni kwa kupitia kwa Kiingereza pekee ambapo Mkenya angeweza kustaarabika.

6. Maandishi haya yalipaswa kufichwa maana ilichelewa kuwa lau yangepatikana watu wangegeuka kuwa Wakomunisti. Hili ndilo waliloliogopa Waingereza.

7. Waingereza walikipa Kiingereza umuhimu mkubwa nchini Kenya. Mtu alihesabika amestaarabika kutokana na ujuzi wake wa Kiingereza. Bila ujuzi huu, mtu alikuwa ni mshenzi. Katika fikira za Wazungu, ni mtu aliyehesabika pekee aliyepaswa kupewa kazi ya afisini. Kazi za aina hii nazo zilimpa mtu kipato kikubwa kilicho-inua hali yake ya kiuchumi.

8. Hapa hatukutaja lugha za Kiarabu na Kihindi kwa sababu idadi ya wazungumzaji wake illkuwa ndogo. Pia lugha hizi hazikupewa umuhimu mkubwa katika suala la lugha nchini Kenya enzi hizo za ukoloni wa Mwingereza.

9. Hii ni kwa sababu wao, kwa kujifunza Kiingereza, waliupata utamaduni wa Kiingereza. Utamaduni huu ni tofauti kabisa na ule wa Kiafrika. Hali hii iliwafanya wayaangalie mambo katika njia tofauti na walivyofanya Waafrika wengine waliokuwa na misingi thabiti ya utamaduni wao.

SURA YA NNE

## 4.0 HALI YA LUGHA NCHINI KENYA BAADA YA UHURU

### 4.1 Utangulizi

Kabla ya uhuru nchini Kenya, Waingereza walikuwa katika tabaka lao kijamii. Hali hii iliwakera Wakenya waliokuwa wameelimika na ndiyo iliyowapa msukumo wa kuanzisha vuguvugu la utaifa lililosababisha kupatikana kwa uhuru mnamo 1963. Baada ya uhuru Kiswahili kilitumika kama ala ya kujirekebishia kisiasa ambapo kilitumika katika utekelezaji wa sera mbali-mbali za serikali[1] Basi lugha hii ilionekana kama kitu kilichobeba utambulisho wa Wakenya kama watu wa jamii moja.

Ni kwa sababu hii ndipo Kiswahili kikapandishwa hadhi na kupewa uamili wa lugha ya taifa. Hivi, mbali na kuwa ingesaidia kutatua tatizo la kuwa na lugha nyingi nchini Kenya, ingeleta umoja nchini na kuzalisha wasomi ambao wangefundisha Kiswahili katika viwango mbalimbali vya elimu. Pia hatua hii ingesawiri waziwazi fikra za Wakenya kiitikadi na kisiasa. Yaani viongozi wapya walikuwa na kazi kubwa mbele yao maana walikuwa wasimamizi wa nchi na watekelezaji wa masuala yaliyoihusu. Basi iliwapasa wawahamasishe Wakenya kwa kuwa kama nyenzo katika lo lote

walilolitaka. Walikuwa na wajibu wa kutenda hili kwa kutumia zana ya kuwajibika kwa kupanga, kusimamia na kuthibiti yote.

Hali hii ilipasa iwe katika uwanja wa lugha pia maana matumizi ya lugha fulani ni dhihirisho la wazungumzaji katika hali zao za kiasili na kijamii katika mazingira fulani.

Kenya ni nchi yenye utajiri mwingi wa lugha. Lakini Kiswahili ni lugha inayotumiwa na idadi kubwa ya watu. Sasa suala ni: Kwa nini lugha hii haithaminiwi sana nchini Kenya?[2] Tunaamini majibu kwa suala hili yamo katika vipengele vitatu. Mwanzo, ni kule kuwa na Kiingereza kama lugha rasmi, Kiswahili kikisemekana kuwa lugha ya taifa. Pili, ni kutokukubalika kidhati kwa Kiswahili sanifu miongoni mwa baadhi ya waongeaji wa lahaja nyingine za Kiswahili; na tatu ni kuzuka kwa lugha ya Sheng[3] Maswala haya yote tunayatazama kama yaliyo ya kisiasa.

## 4.2 Kiingereza na Uimarikaji wa Kiswahili

### 4.2.1 Msingi wa athari za Kiingereza kwa uimarikaji wa Kiswahili.

Hali ya lugha nchini Kenya ina misingi yake katika aina ya elimu ambayo Wakenya walipewa na wakoloni wa

Kiingereza. Hii ni kwa sababu mfumo wa elimu wa Kizungu ulizalisha wasomi ambao thamani yao ilitegemea kiasi cha kuimarika kwao katika Kiingereza. Kuimarika huku katika Kiingereza kuliwafanya kuwa katika tabaka lao, kando na la wale waliokuwa na umilisi na lugha ya Kiswahili na lugha zile nyingine za kikabila. Wakati huo wa ukoloni, matumizi ya ama Kiingereza au Kiswahili yalimfanya mtu aeleweke kwa njia fulani, na apewe hadhi fulani, katika jamii.

Harakati za kudai uhuru zilipowadia, kulizuka mtazamo wa kidhati kuhusiana na masuala ya kitabaka kama haya. Hata hivyo, hata baada ya Kenya kujipatia uhuru, hapana mageuzo mengi yaliyofanywa kuhusiana na hali ya lugha. Tungetaraji kuwa kutokana na maendeleo mapya katika siasa za Kenya zenye misingi katika demokrasia - ambayo huhubiri dhana ya uwakilishaji - lugha ya walio wengi ndiyo ingetumika kwingi kidhati. Sababu yake, kama ambavyo tumekwisha kutaja, ni ile hali ya kuwa na Kiingereza kama lugha rasmi huku Kiswahili kikitumika kama lugha ya taifa tu.

Msingi wa hali hii u katika historia ya lugha hizi mbili. Katika historia ya Kenya, suala la biashara ya watumwa na la kusambazwa kwa Kiswahili yana mafungamano fulani kwa sababu lugha hii ndiyo iliyo-kuwa chombo cha mawasiliano baina ya wafanya biashara ya watumwa na watu wa bara waliokuwa wamegawanyika

kimakabila. Wakoloni wa Kiingerreza wakijua vizuri sana kuwa Wakenya walifahamikiwa kwa hili, waliwashawishi watumie lugha zao za kikabila katika shughuli kama vile za kidini na za kielimu. Nia yao hasa ilikuwa ni kujaribu kuvunja ule uwezekano wa Wakenya kuja pamoja kwa kuzungumza lugha moja iliyowaunganisha. Nacho Kiingereza kilifunzwa wachache ambao walifanywa kujihisi kwamba walikuwa bora ikilinganishwa na wale wengine. Hali hii ilizalisha kundi la Wakenya waliouhusudu Uzungu katika vipengele vyake vyote, kikiwemo kile cha lugha.

Kwa sababu hii, taifa jipya la Kenya baada ya uhuru lilizidi kuhimiza matumizi ya Kiingereza. Hali hii ilijilazimisha maana wakati huo Wakenya wenyewe walikuwa hawakumakinika katika masuala mengi yaliyowapasa kuyatekeleza kama watu huru. Kwa kuwa hawakutaka taifa lao jipya liangamie wakawa hawana budi kujizoazoa pole pole kwa kuwa na ushirikiano, ukiwemo wa kilugha, na waliokuwa wakoloni wao. Yaani, hali ya lugha iliyoonekana katika nyakati za wakoloni ilibebwa hadi Kenya huru. Kama ilivyokuwa katika enzi ya wakoloni, Kenya huru pia imekuwa na migao kati ya wale waliobobea katika Kiingereza na wale wanaozungumza Kiswahili na lugha nyingine za kikabila.

4.2.2 Elimu na Uimarikaji wa Kiingereza dhidi ya Kiswahili

Hali hii tuliyoiongelea hapo juu imesababishwa na aina ya elimu wanayopewa Wakenya. Mbali na kuwa elimu hii inasisitiza Kiingereza, hunuiwa kumbadili mwana wa mkulima kijijini awe ni mtegemea mshahara. Nayo mishahara, kwa mujibu wa sera ya uajiri nchini Kenya, hupewa wale watu walioelimika - ambapo kuelimika kuna maana ya kuwa na cheti safi ambacho hakikuathiriwa na kufeli kwa Kiingereza mitihanini.

Basi wale wanaozungumza Kiswahili, na ambao pia ni wa ngazi za chini kijamii, hawaruhusiwi maingiliano ya moja kwa moja na wale wenye kuzungumza Kiingereza. Ni kwa sababu hii ndipo kuna ilani 'Mbwa kali' katika mitaa kama vile Kileleshwa na Muthaiga mjini Nairobi. Dhana hii ya 'Mbwa Kali' ilianzishwa na Wazungu ambao, kwa kutowajibika, hawakujali sarufi ya Kiswahili. Hali hii imekuwa na lengo la kuyatenga kabisa makundi haya mawili, ambapo moja latumia lugha ya walio wengi huku jingine likitumia lugha ya wateule wachache. Hali hii inamaanisha kuwa Kiswahili kitaendelea kuwa lugha ya walio wengi nchini Kenya huku Kiingereza kiking'ang'aniwa na wachache wenye 'bahati' ya kukitumia, na kwa ufasaha. Hii ni kwa sababu ujuzi wa Kiingereza unamaanisha kuelimika vyema kinyume na ujuzi wa Kiswahili.

### 4.2.3 Uchumi wa Uimarikaji wa Kiingereza dhidi ya Kiswahili

Kwa jumla, Kiingereza kimeonekana kuwa ni lugha nzuri na yenye matumaini kuliko Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru. Hili limekuwa hivi kwa sababu ya yale manufaa ya kiuchumi na kijamii yanoyoambatishwa na lugha hii 'tukufu' - Kiingereza.

Kihistoria, Kiswahili kimekuwa kikifungamanishwa na watumwa, wageni katika janibu za Afrika ya Mashariki, watu wasio asili wala fasili, na - la mno - wafanya kazi za sulubu. Bila shaka hii ndiyo sababu ya hali ya Kiswahili kuwa ilivyo nchini Kenya. Ye yote atakaye kazi ya 'tepenyeupe' hana budi kuwa amehitimisha kiwango fulani cha elimu na ana ujuzi wa Kiingereza. Hali hii humtayarisha mtu kuingia katika tabaka la kijamii lililo jipya na lenye maslahi zaidi. Kwa sababu hii mtu abahatikaye kuingia tabaka hili la kijamii hujibidiisha kubadilika katika tabia zake, zikiwemo zile za kilugha, ili kuingiliana barabara na matakwa ya tabaka lake.

Yaani tabaka ni mbinu muhimu sana katika harakati za kuchagua lugha fulani itumike mahali fulani kwa madhumuni kadhaa. Wakenya wengi wajihisio kuwa wameelimika, na kwa hivyo wanajiweza kiuchumi, hukitumia Kiingereza hata pale wanapokuwa na uhakika kuwa hadhira yao haielewi Kiingereza vyema. Hili hufanywa

ili kuidhihirishia hadhira yao hadhi yao (waongeaji) maana Kiingereza kimekuwa ni njia majowapo ya kuudhihirisha utukufu wa mtu nchini Kenya. Katika hali hii lugha, kama chombo cha mawasiliano, hukosa maana kabisa. Aghalabu watu kama hawa watasema wanakitumia Kiingereza kwa sababu ni lugha rasmi nchini Kenya. Lakini katika kujitetea hivi, daima tukumbuke kuwa yale majukumu rasmi anayopewa mtu huwa ni kwa ajili ya wananchi wote na wala sio wachache wafahamuo Kiingereza. Kwa hivyo lazima mtu atumie lugha itakayomwezesha kuwasiliana vyema na wananchi wengi wa Kenya.

Tuonavyo ni kwamba hali hii ipo kwa sababu ya kuwa na Kiingereza kama lugha rasmi huku Kiswahili kikisemekana kuwa ni lugha ya taifa bila kila mojawapo ya lugha hizi kupewa mpaka wa majukumu yake. Kinachoonekana basi ni watu kubambanya bambanya tu matumizi ya lugha hizi kwa kurejelea historia ya matumizi ya lugha hizi nchini Kenya.

Kenya ilipojinyakulia uhuru wananchi wake walitaka kuuhifadhi utamaduni wake kwa kuurekebisha pale ambapo ulikuwa umepotoshwa na wakoloni. Lugha ya Kiswahili ni moja ya sura za kiutamaduni nchini Kenya. Kwa Mkenya asiye na kisomo, lugha hii ndiyo ilikuwa sauti yake katika kuwasiliana na Wakenya wengine maana ilikuwa yaeleweka na kuzungumzwa kote

kutokana na kuwa kwake lingua franka katika Afrika ya Mashariki na ya Kati. Kwa upande mwingine, wale Wakenya waliokimudu Kiingereza walisumbuliwa sana na ile hoja kuwa Kiswahili kingekuwa na uzito zaidi katika juhudi za kuufufua utamaduni wa Waafrika nchini Kenya. Ilikuwa imewagharimu mengi kujifunza na kubobea katika Kiingereza.

Watu kama hawa - akiwemo aliyekuwa wakati mmoja mwanasheria mkuu wa Kenya Bwana Charles Njonjo - si ajabu, wamefanya juu chini kukipa Kiswahili 'mahali pake' kwa kuzitoa 'kasoro zake' ambamo mna hoja kuwa lugha hii haijitoshelezi kimawasiliano maana ni pungufu kimsamiati kiasi cha kutoweza kukabiliana barabara na hali ya ulimwengu leo uliojaa matukio ya kisayansi na kiteknolojia. Hoja kama hizi zilikuwa (na zina) misingi katika ubaguzi wa kijamii na wala si ithibati za kiisimu. Kusema kuwa Kiswahili ni lugha pungufu kimsamiati ni kuchukulia kuwa haina uwezo wa kukua ilhali ni ukweli-dhahiri kuwa lugha yo yote inapoingiliana na nyingine kama kilivyo Kiswahili huathiri na kuathiriwa. Haikosi ni kwa sababu ya propaganda za aina hii ndipo Kiingereza kikafanywa lugha rasmi nchini Kenya mara tu baada ya uhuru nacho Kiswahili kikafanywa lugha ya taifa baadaye kidogo na bila ya kupewa majukumu maalumu.

### 4.2.4 Urasmi wa Kiingereza na Uimarikaji wa Kiswahili

Kwa kuwa Kiingereza ndiyo lugha rasmi ya Kenya, yatumika katika maafisi yote ya serikali. Pia, ili kukiimarisha zaidi kama lugha muhimu, Kiingereza kinapewa muda mwingi wa kufunzwa katika shule za Kenya.[4] Licha ya kuwa Kiingereza kinavyo vitabu vingi vyenye thamani viandikwavyo kukihusu (na katika lugha hii) ikilinganishwa na vile vya Kiswahili, pia vipindi vyake katika T.V. ya Kenya ni vingi vikilinganishwa na vile vya Kiswahili. Hizi ni baadhi tu ya juhudi za kimsingi ambazo huwapa Wakenya mshawasha wa kukihusudu Kiingereza. Hata hivyo, huku kusukumiziwa Kiingereza hakusisimui hisia zao za kukipenda au kukitumia kidhati ingawa huwaelekeza wengi wao katika kukifahamu kinapokuwa kinatumika katika maongezi ya kijumla. Lakini, kwa sababu ya ule utabaka wa juu ambao lugha hii huambatana nao, watoto wanapofunzwa Kiingereza shuleni hukipata mara moja.

Bila shaka sera ya kikoloni nchini Kenya ambayo iliweka mpaka kati ya maingiliano ya kilugha na kijamii baina ya Waafrika na Wazungu ndiyo sababu kuu ya Wakenya kukichukua Kiingerreza kama lugha yao rasmi baada ya kujipatia uhuru. Waingereza waliwaathiri Wakenya kifikira walipoanzisha mifumo ya elimu na sheria ambazo zilizuia na kubana kufunzwa kwa Kiswahili na hivi wakahujumu maendeleo ya lugha

hii. Matokeo yake yalikuwa kule kuipa umadhubuti lugha ya Kiingereza. Baada ya uhuru basi, Kiingereza kilibakia lugha ya kufunzia katika karibu viwango vyote vya elimu ili kutayarisha wanafunzi kufanya kazi mahali rasmi nchini.

Hata hivyo, Kiswahili hakikupuuzwa. Mnamo 1974 ilipitishwa bungeni kuwa Kiswahili kiwe ni lugha ya taifa na pia itumike sambambba na Kiingereza katika kujadili masuala ya bunge. Na kufutia hatua hii, ili kuingia bunge sharti mtu apasi mtihani katika lugha zote mbili: Kiingereza na Kiswahili. Lakini kutoka 1974 maamuzi haya yalipofanywa ni machache sana ambayo yamefanywa ili kuimarisha matumizi ya lugha hii ya Kiswahili katika bunge. Kutokana na hali hii mtu anaweza kujiuliza masuali kama yafuatayo: Je, katika kujitahidi kuupita mtihani wa Kiswahili wajumbe hujilazimisha tu ili wasionekane kuwa ni watu walio kando na watu wanaowawakilisha?, Je, maamuzi haya yalikuwa ni mazungumzo tu ya kawaida ya wanasiasa au yalilenga katika kuihasiri sehemu fulani ya umma wa Wakenya? n.k. Kama tulivyoona, Wakenya wangali na Kiswahili kama lugha ya taifa nacho Kiingerza ni lugha rasmi. Pia tumetaja kuwa kila mojawapo ya lugha hizi haikutengewa majukumu maalumu na yaliyo wazi. Kutokana na hali hii, hali ya ukinzani imezuka ambapo Uingereza (na ulimwengu wa Kimagharibi kwa jumla) yapigania matumizi zaidi

ya Kiingereza dhidi ya Kiswahili. Hii ndiyo sababu si ajabu kupata Wakenya wanapewa udhamini wa kwenda kusomea Kiingereza huko Uingereza au Waingereza wanakuja katika vyuo vya Kenya ili kufunza tamrini za lugha ya Kiingereza. Jambo hili si geni katika historia ya lugha nchini Kenya maana katika enzi ya ukoloni wa Mwingereza

> ... wengine kama vile Mheshimiwa Bemister waliopenda kuwe na himaya yenye kuzungumza Kiingereza walitka kuhimiza Kiingereza. Hoja ... zililtiwa motisha na mitazamo ya kisiasa badala ya kielimu.[5]
>
> (Tafsiri Yetu)

Yaani hapa tunakitazama kitendo hiki cha kuwa na wasomi teule walioimarika na kumakinika katika Kiingereza baada ya kufunzwa na Waingereza au baada ya kwenda kujifunza Uingereza kama kilicho cha kisiasa. Hali hii hutokana na presha inayotokana na ile hali ya kuwa na Kiingereza kama lugha rasmi na Kiswahili kama lugha ya taifa. Kunakuwa na mashindano katika matumizi ya lugha hizi mbili.

Ingawa lugha rasmi na lugha ya taifa zina ufanya kazi ulio tofauti, ni fikira yetu kuwa ili kuichukua lugha na kuitukia katika muktadha fulani lazima watu wanaoichukua kukubali yote yanayoambatana na utamaduni wa lugha hiyo. Maamuzi, basi, ya ikiwa

Kiingereza kitaendelea kuwa lugha rasmi huku Kiswahili kikiwa lugha ya taifa hayana budi kuwa na misingi katika kukubalika kwa kila mojawapo ya lugha hizi katika siku za usoni. Daima tukumbuke kwamba tofauti za kijamii hazipaswi kuwa ndizo zinazowaelekeza Wakenya katika kuchagua lugha za matumizi; lakini wachague lugha ambazo zitaingiliana vyema na hali yao ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, na kihisia.

Mambo hayawezi, kuwa hivi kwa sababu ya siasa za lugha. Wakoloni waliwang'oa waafrika kutoka katika mizizi yao ya kiasili. Katika kufanya hivi waliwa kengeusha kiasi cha kuwafanya waamini kwamba kila kilicho cha mtu mweupe ni bora kikilinganishwa na kile cha mweusi. Baada ya uhuru, ingetegemewa kuwa uzalendo ungewaongoza Wakenya katika masiala yao kuhusu lugha. Mageuzi katika mpango wa lugha yangekuwa jambo muhimu na la lazima ambalo halingekuwa la kitaifa tu bali la kijamii pia. Isingetarajiwa viongozi kujitenga kilugha na kijamii kutoka kwa wale waliowawakilisha kwa kuwa na Kiingereza kama lugha rasmi na Kiswahili kikiwa lugha ya taifa.[6] Hata hivyo, isichukuliwe kuwa hiki ndicho kikwazo cha kipekee kwa uimarikaji wa Kiswahili nchini Kenya. Kuna hili suala la Kiswahili Sanifu kutokukubalika kidhati miongoni mwa baadhi ya waongeaji wengine wa Kiswahili nchini Kenya.

## 4.3 Lahaja za Kiswahili na Uimarikaji wa Kiswahili

Baadhi ya wazungumzaji asilia wa lugha ya Kiswahili na ambao lahaja zao si Kiunguja hawakiheshimu Kiswahili Sanifu. Wao watakiita majina mbalimbali ambayo yana bezo ndani yake. Kwa nini hali iwe hivi? Na je, hali hii ina athari gani katika uimarikaji wa Kiswahili nchini Kenya? Haya ndiyo maswali tunayojibu katika kijisehemu hiki.

### 4.3.1 Vita vya Lahaja Muhimu Uswahilini

Wamisheni walipokuwa wanayashughulikia masuala ya elimu nchini Kenya, walikabiliwa na tatizo la ni lugha ipi ambayo ingefaa zaidi katika kazi hii, hasa kwa upande wa elimu ya waafrika. Baada ya muda wa kushauriana na serikali, ilionekana kuwa ni lugha ya Kiswahili ambayo ilisadifu zaidi katika shughuli hii. Sasa suala lililozuka lilikuwa kuhusu lahaja ya Kiswahili ambayo ingechaguliwa na ambalo lilijitokeza na wazo la kukisanifisha Kiswahili. Lahaja ya Kiunguja ilijishindia wadhifa wa kuwa msingi wa kusanifishia lugha ya Kiswahili ambayo ingetumika kote kama Kiswahili Sanifu.

Hata hivyo, baada ya Kiunguja kuchaguliwa, kulizuka pingamizi mbalimbali kutoka kwa wazungumzaji wa baadhi ya lahaja nyingine za Kiswahili. Sababu mbalimbali zimetolewa kuhusiana na pingamizi hizi lakini tunaamini kuwa zote ni visingizio tu maana

kisa hasa ki katika hali za kijamii na kisiasa ambazo zahusika miongoni mwa wasemaji wa baadhi ya lahaja nyingine za Kiswahili. Kwa Kiunguja kuchaguliwa, wamehisi kwamba wao wamebaguliwa. Hali hii imewabidi wakipige vita Kiunguja. Kumezuka hali ya kushindana kilahaja, hasa kutoka kundi ambalo lahaja zake zilipuuzwa katika shughuli ya upataji msingi wa kusanifishia lugha ya Kiswahili.

Wale Waswahili wanaokipinga Kiswahili Sanifu wanapuuza hoja kuwa lugha fulani inapochaguliwa miongoni mwa nyingine, haina budi kutimiza matakwa ya wengi. Hivi ndivyo kilivyokuwa Kiunguja kwa namna kilivyokuwa kimeenea. Lakini Waswahili hawa wamekiona Kiunguja kama kilichopendelewa. Kwa sababu ya 'mapendeleo' haya, wanahisi Waunguja wanatazamwa kama walio watu muhimu kuliko wazungumzaji wengine wote wa lajaha nyingine za Kiswahili maana ndio wanaoshikilia kaida ya uzungumzaji wa Kiswahili.

Pingamizi za aina hii ni za kilimwengu na wala zisichukuliwe kuwa ni kwa Kiswahili pekee. Kuliko na makundi yaliyogawanyika kijamii, hali hii haina budi kutokea. Pingamizi kama hizi huwa nyingi zaidi pale lugha zinapokuwa na umbali mkubwa. Baadhi ya wale wasioongea lahaja sanifu huhisi kuwa lahaja hiyo inasukumizwa ili kuchukua mahali pa lahaja nyingine

zote. Ni kwa sababu hii ndipo baadhi ya Waswahili wamekihusudu sana Kiunguja. Bila shaka wao huhisi kuwa ni kwa kupitia lahaja hii ndipo Kiswahili kimetolewa pwani na kufanywa lugha ya kimataifa.

Husuda hii dhidi ya Kiunguja imezusha vita vya 'lahaja muhimu' Uswahilini na baadhi ya wazungumzaji wa lahaja fulani za Kiswahili hawataki kukubali kuwa vita vimekwisha kushindwa na Kiunguja. Kwao, kukubali Kiunguja kutaaminisha wamekubali huo uchaguzi. Kwa kuwa suala la uchaguzi huenda na mipango na maslahi yaliyokusudiwa, wamekataa kuikubali lahaja hii. Wao wanauona uchaguzi huo katika mitazamo ya kiuchumi, kiutamaduni, na kisiasa.

### 4.3.2 Kiunguja na maslahi kwa waongeaji wake

Lahaja ni sehemu ya lugha. Lahaja, kama zilivyo lugha, zina uwezo wa kujisimamia kama vyombo vya mawasiliano. Lahaja moja inapoteuliwa kama ambavyo Kiunguja kiliteuliwa miongoni mwa lahaja nyingine za Uswahili huwa na maana kuwa ndicho chombo kilichokubaliwa na kupewa idhini, miongoni mwa lahaja nyingine, ili kuwa msingi wa cho chote kitachofanywa kuhusu lugha hiyo. Kwa sababu hii, wale watumiao chombo hiki hupewa hadhi na staha ambazo wazungumzaji wa lahaja nyingine huwa hawana. Ili kufaidi maslahi haya inawabidi waongeaji wa lahaja nyingine wajirekebishe na wakiige chombo hiki 'chema'. Ikiwa wazungumzaji wa lahaja nyingine

hawatajirekebisha hivi watakosolewa katika uzungumzaji wao hata na wageni walio na umilisi wa lahaja sanifu.

Katika hali kama hii, wazungumzaji asilia wa lahaja iliyofanywa msingi wa kusanifishia lugha yao watajihisi bora. Basi, kuzungumza lahaja sanifu kunakuwa ni kitambulisho cha mtu aliyeelimika na hata kustaarabika. Ni kwa matumizi ya lahaja hii ndipo mtu anaweza kuuelezea utamduni wa Waswahili ukaweza kueleweka na wengi. Kwa hivyo kuzungumza lahaja hii kuna maana kuwa mwongeaji ni mtu anayejitambulisha na umma mkubwa unaojitambulisha na lugha hiyo.

Ni lugha sanifu itumikayo katika shughuli za kielimu. Nayo elimu waipatayo watu shuleni imetumika kama chombo cha kunasia kazi kwingi ulimwenguni. Halafu mtu apatapo kazi hivi, haitegemewi kuwa mshahara wake utakuwa sawa na ule ambao mtu asiye na kisomo atapata. Hali hii nayo itampeleka mtu katika ngazi ya juu kijamii. Yaani mtu asipotumia lahaja sanifu katika mianda rasmi au ya kitaifa anaweza kunyimwa maslahi kama vile kazi, nyongeza za mishahara, na kupanda ngazi kazini.

Ni katika misingi hii ndipo baadhi ya wazungumzaji wa lahaja nyingine za Kiswahili wamekihusudu Kiswahili Sanifu. Hali kama hii inaweza kuathiri maendeleo na uimarikaji wa lugha yo yote ile. Tukirejelea

Kiswahili , watu wasio Waswahili wanaweza kuitumia hali hii kama kisingizio cha kutoithamini. Na hivi ndivyo hali ilivyokuwa nchini Kenya katika miaka ya sabini watu wa makabila ya Kinailotiki walipokipinga na kukisema Kiswahili kuwa ni lugha ya kisuriama na ambayo haingeweza kuusawiri vyema utamaduni wa Kenya kama ingefanywa lugha ya taifa (A.A. Mazrui, 1972:89).

Hata hivyo, Kiswahili kimezidi kuimarika kila uchao. Ni katika miaka ya hivi karibuni ambapo lugha-pendwa kwa jina la Sheng' imezuka nchini Kenya na huenda ikaathiri maendeleo na uimarikaji zaidi wa Kiswahili kama lugha ya kimataifa.

## 4.4 Athari za Sheng' katika Kiswahili

### 4.4.1 Nadharia zihusuzo chimbuko la Sheng'

Nadharia mbalimbali zinaweza kutolewa kuhusu chimbuko la lugha hii ya Sheng'. Nadharia moja ni kuwa Sheng' imezuka vivi hivi tu kwa sababu ya kimtindo ambapo wazungumzaji wake wametaka kujitokeza na lugha iliyojaa madoido. Yaani msingi wa lugha hii si kuwasiliana maana watu wanaoitumia wana na lugha nyingine ambazo ni vyombo imara vya mawasiliano ambavyo vimepata misingi na maimarisho kutokana na muda mrefu wa kutumika kwake. Ni kwa sababu hii ndipo Sheng' si pijini bali aina ya lugha -

vipindi kwa jinsi ambayo msamiati wake hubadilika kila uchao.

Huu ni mtazamo mmoja. Mtazamo wa pili na ambao kwetu una mashiko zaidi, wahusu mahali pa kuchimbuka kwa lugha hii ya Sheng'. Lugha hii imezuka katika miji ya Kenya miaka ya hivi karibuni. Ni watoto wa wafanyakazi wa kisasa mijini wanaoweza kusemekana kuwa ndio waanzilishi wa lugha hii. Sababu ya kuzuka kwa lugha hii, kwa maoni yetu, ni ya kisaikolojia. Watu hawa hawangeweza kukubalika katika tapo la wale wanaotawala[7]. Kwa hivyo, walihisi walikuwa wanadhulumiwa kwa sababu ya lugha kila mmoja wao aliyo na umilisi nayo. Yaani kwao, tofauti kubwa za mapato baina ya Wakenya 'wenye navyo' na "waso navyo" zimesababishwa na lugha. Watoto hawa wa wafanya kazi wa mijini kimsingi, ni watumizi wa Kiswahili nao watawala na watoto wao ni watumizi wa Kiingereza safi. Basi watoto wa wafanya kazi hawa walijitokeza na Sheng' ili iwe ni kama mkakati wa kisiasa wa kupigana na watawala kwa kutaka ushirikiano wa makundi yaliyoko vijijini na ambayo yako katika hali mbovu zaidi ya haya mengine ya mijini.

Kama alivyosema Karl Marx, wale katika jumuia ya wafanya kazi walio afadhali kidogo ndio ambao hujitwika jukumu la kuwaongoza wenzao katika harakati zo zote za kimapinduzi. Hili ndilo walilolifanya waasisi wa

Sheng' na ambao ni watoto wa wafanya kazi wa mijini. Ingawa wapo mijini, wanahisi kuwa wao si sawa na wale walio na uwezo wa kisiasa na kiuchumi kwa sababu kwao, kutokana na hadhi zao lugha ya mawasiliano ni Kiingereza ambayo ni lugha ya kimataifa zaidi kuliko Kiswahili, na hata watoto wao huhudhuria masomo katika shule zilizo za watu wa kimataifa. Hawa ndio watu watumiao Kiingereza safi. Ingawa watumizi wa Sheng' wapo mijini, makazi yao, tabaka za shule wanazosomea, 'uhuru' walio nao, n.k ni vitu ambavyo haviwaruhusu kukata mafungamano na wenzao walioko vijijini. Kwa mfano kinyume na watoto wa tabaka tawala ambao huenda hata wakaagiziwa vyakula kutoka ng'ambo, watoto wa tabaka hili la wafanya kazi (na linaloweza kuitwa la kati) hupata baadhi ya vyakula kutoka vijijini. Basi lugha ya Sheng' imejitokeza kama lugha ya kuwa-unganisha Wakenya wote kwa juhudi za wafanya kazi wa vijini.

Tunasema hivi kwa maana tunaamini kuwa waanzilishi wa Sheng' waliiona hali ya lugha nchini Kenya kama iliyo na kasoro kwa jinsi ambayo iliwatia watu katika makundi ya kijamii, kutegemea uwezo wa mtu kilugha. Ni kwa sababu hii ndipo tumetoa kauli kuwa ni vita vya kisaikolojia ambayo vimezalisha lugha ya Sheng'. Bila shaka waliyaona matumizi ya lugha katika Kenya huru yakifanana sana na yale yaliyokuwa ya Kenya ya kikoloni na kwa hivyo wakataka kuleta mageuzo fulani.

Ikiwa kweli mambo yako hivi, suala ni namna lugha ya Sheng' itakavyosaidia katika kuunda Kenya isiyo na lugha ambazo ni hifadhi za watu wa matabaka fulani pekee.

### 4.4.2 Sheng' na uimarikaji wa Kiswahili

Baada ya kusema haya maneno ya ufunguzi kuhusu Sheng' ni muhimu tukumbuke kuwa tunachambua athari zinazoweza kutokea kwa uimarikaji wa Kiswahili nchini Kenya kutokana na kuzuka kwa Sheng'. Tunatazama vipengele hivi vifuatavyo kufungamana na Sheng' ili tuweze kusema ni vipi ambavyo kila kimoja wapo kina athiri Kiswahili: fonolojia, msamiati, mofolojia, na sarufi.

Fonolojia ya wazungumzaji wa Kiswahili na ile ya waongeaji wa Sheng' ni tofauti. Tofauti hii haijitokezi waziwazi katika mifumo ya vokali ya lugha hizi lakini mifumo ya konsonanti yaonyesha tofauti hizi. Wazungumzaji wa Sheng' wanao wingi wa konsonanti.[8] Kwa sababu hii, wao wana uhuru wa kuyatamka maneno wapendavyo bila kozongwa na sheria kali za kifonolojia. Pia, konsonanti hizi huungana kwa njia mbalimbali kutegemea lugha ambayo kwayo msamiati huo huwa umechukuliwa. Kwa sababu hii Sheng' ina uwezo wa kuunda msamiati mwingi ipendavyo.

Mikopo ya maneno kutoka Kiingereza ni sura muhimu ya lugha ya Sheng'. Hata hivyo, muundo wake kimsingi

ni wa Kiswahili ingawa sheria za uundaji wa misamiati zitumikazo katika Kiswahili hukiukwa hapa na pale. Ili kuelewa lugha hii basi, mtu hana budi kuwa na ujuzi, angaa mdogo, wa Kiingereza na Kiswahili.

Nayo tofauti muhimu ya kisintakisia kati ya Sheng', Kiswahili na Kiingereza ni ile hali ya Sheng' kuwa imerahisishwa. Waongeaji wa Sheng' aghalabu huwasiliana kwa matumizi ya sentensi fupi fupi ambazo huwa hazina utata wo wote wa kisarufi. Labda ni ile hali ya msamiati wake kukosa kuwa wa kudumu inayowaongoza wazungumzaji wa Sheng' katika kuwasiliani hivi. Sifa hii ya kukosa msamiati wa kudumu huifanya Sheng'kuwa ni lugha ya kimuktadha zaidi, kinyume na Kiswahili.

Kwa maoni yetu, Sheng' ni lugha-msimu, ya Kiswahili. Kwa kuwa wazungumzaji wa Sheng' wanaongezeka kila uchao, hali hii itakifanya Kiswahili kuwa na Uzungu mwingi sana katika msamiati na hata muundo wake. Hivi, lugha ya Kiswahili inaweza kuathiriwa kama chombo kibebacho utambulisho wa taifa la Kenya. Pia hali hii itafanya Kiswahili kikosolewe kama lugha iliyo ya mchanganyiko na isiyojitosheleza kimsamiati ila kwa kudowea kwingineko bila mpango maalumu. Katika hali kama hii, ni watu wachache sana watakaotaka kukijua na kukiongea Kiswahili hadharani. Badala yake, watahiari kujifunza na kuongea Kiingereza ambacho, kiulinganishi, ni lugha madhubuti, iliyojaa fahari, na

ya kimataifa zaidi. Na ikiwa matumizi ya Kiswahili yatapungua hivi, hii itakuwa na maana kwamba Wakenya watakuwa wanapoteza kitambulisho chao cha kitaifa wakibobewa katika utamaduni wa Kimagharibi unaosimamiwa na Kiingereza.

## 4.5 Hitimisho

Viongozi wa Kenya huru wanahitaji kuuleta umoja wa kitaifa nchini. Wakati huo huo wanalenga katika kuiendeleza nchi yao kiuchumi. Wangependa kuwaona watawaliwa wakiwa katika hali nzuri katika vipengele vyote vya maisha. Hata hivyo, ili kupata hali hizi inawabidi Wakenya kuwasiliana vyema na nchi zilizo-endelea. Ni kwa sababu hii ndipo kunakuwa na usisiti-zaji wa Kiingereza katika mifumo ya elimu ya Wakenya. Hali hii huwa na athari za kukififisha Kiswahili na lugha nyingine za kikabila katika kuimarika kwake. Yaani kuimarika kwa Kiswahili nchini Kenya kumeathiriwa na ule umuhimu unaopewa Kiingereza ikilinganishwa na lugha nyingine.

Ili kuhakikisha kwamba Kiingereza kinatumika kidhati, serikali imejitokeza na vivutio vilivyojengeka katika maslahi na faida za kiuchumi na kijamii kwa wale wanaobobea katika Kiingereza. Ni hivi ambavyo lugha hii ya Kiingereza hukua kila uchao kwa kujipatia waongeaji zaidi. Kwa upande mwingine, maslahi na faida za kiuchumi na kijamii ambazo huenda na Kiswahili Sanifu husaidia katika kukitweza

Kiswahili nchini Kenya. Mvutano wa ikiwa Kiunguja kilichaguliwa kihalahi, ikiwa kinafaa au la, n.k huwakatisha tamaa baadhi ya watu kujifunza lugha hii.

[Pia hali hii ya watu kujihisi wanyonge na duni kilugha imeathiri vikubwa kuimarika kwa lugha ya Kiswahili baada ya uhuru nchini Kenya. Kama tulivyokwisha taja, wengi wa Wakenya huhisi kuwa Kiingereza ni lugha bora ikilinganishwa na Kiswahili. Ni kwa sababu hii ndipo wengi wao wanahiari Kiingereza dhidi ya Kiswahili. Pia ni kutokana na hali hii ndipo lugha ya Sheng' imezuka ili kujaribu kuvunja kasi za Kiingereza kwa kuwa na lugha iliyo rahisi na ya kimuktadha zaidi. Hapa suala ni: Je, lugha hii husaidiaje katika kuboresha Kiswahili?]

## 4.6 Tanbihi

1. Kilikusudiwa kuufanya umma mkubwa wa Wakenya ufikirie kuwa viongozi wao walikuwa nao na waliwajali ndipo wakaamua kutumia lugha ambayo wangeelewa vyema.

2. Wakenya wengi, hasa walio na uwezo wa kiuchumi na kielimu, hawapendi kukiongea hadharani. Hata maskini wanapokuwa katika hali ya furaha watasikika wakibobojekwa na maneno ya Kiingereza.

3. Ni ukweli-dhahiri kuwa Kiswahili Sanifu hakikubaliki kidhati kote Uswahilini. Ni kwa sababu hii ndipo si ajabu kuwasikia baadhi ya wazee wa Kiswahili wakikiita kiserikali. Hata wengine kama vile Khalid, Abdallah wanaandika vitabu ili kukiponda. Hali kama hii inaweza kuathiri kukua kwa Kiswahili Sanifu.

4. Huenda hoja hii isikubalike na wafanya kazi wa Taasisi ya Elimu Kenya (KIE) maana kwao Kiingereza na Kiswahili ni masomo yaliyo na vipindi sawa kwa juma. Hata hivyo, waalimu wakuu wa shule mbalimbali, wakishirikiana na wasimamizi wa vipindi shuleni mwao huchukua baadhi ya vipindi vya Kiswahili na kukipa Kiingereza.

5. Haya ni maneno ya T.P Gorman (1974) ambaye anatazama suala la kuenezwa kwa Kiingereza kama lililo la kisiasa.

6. Kuna kitu katika akili ya binadamu ambacho humfanya kuuliza: Kwa nini? Sasa Wakenya hujiuliza mbona Kiingereza kimefanywa lugha rasmi ili kitumike katika maafisi ya serikali na mahali pengine rasmi nacho Kiswahili kimefanywa lugha ya taifa ili kiweze kutumika

katika mawasiliano ya kivivi hivi tu na yasiyo rasmi? Katika hali kama hii watu hawawezi kukichukulia Kiswahili kidhati.

7. Kama ilivyo katika mahali po pote palipogawika kimatabaka, nchini Kenya kuna migao ambayo husawiri ngazi ya mtu kijamii. Kimakazi mijini, wachochole watapatikana katika mitaa kama vile Mathare na Kibera Laini Saba, watu wa tabaka la kati watapatikana katika mitaa kama vile Buruburu, na watu wa ngazi za juu (ambao wana watawala ndani yao) watapatikana katika mitaa kama vile Lavington. Katika mitaa ya watu wa tabaka la juu, kama tulivyo-kuisha taja, lugha ya mawasiliano ni Kiingereza safi. Kwa kuwa watoto wa watu hawa hawaruhusiwi maingiliano na watu kutoka matabaka haya mengine, lugha yao imebakia kuwa ni Kiingereza safi.

8. Tunasema hivi maana tajriba yetu imetuonyesha kuwa wazungumzaji wa Sheng' wana uhuru wa kuchota msamiati kutoka lugha yo yote ile na kuutumia bila ya kuupurura au kuufanyia mageuzo yo yote.

SURA YA TANO

## HITIMISHO

Katika kazi hii, tumejaribu kuonyesha jinsi Kenya huru ilivyorithi na kuhifadhi asasi za utabaka zilizoasisiwa na wakoloni wa Kiingereza. Katika kuitia hali hii katika muktadha wa kilugha tumepata kuwa hali hii ya kudunisha lugha fulani kwa kuiendeleza nyingine haikufaulu. Kauli hii ni kwa mujibu wa mtazamo wetu. Kwa kuwa kuna mitazamo mingi kama tulivyo na watu wengi, hatuna budi kusema kuwa kwa haya tuliyoyasema tumekusudia kuchochea mijadala zaidi kuhusu lugha nchini Kenya.

Hata hivyo, nia yetu ya kushughulikia anwani 'Siasa na Uimarikaji wa Kiswahili' ilikuwa ni kuwahamasisha wasomi wa Isimu-jamii-hasa wanaojishughulisha na lugha za kiafrika-ili waweze kuzitafiti lugha za kiafrika na kuzalisha uelewa fulani kuzihusu. Hivi, fikira-potoshi kuhusu lugha za kiafrika kama vile kutojitosheleza kimsamiati zitapigwa vita kwa usaidizi wa tafiti zenye kina na maki katika lugha mbalimbali.

Tulipoanza kazi hii tulidhani kuwa hatungekuwa na mengi ya kujadili lakini baadaye tumetambua kuwa hii ni mada iliyo na mengi. Hasa tumegundua mada hii yaweza kugawika katika sehemu tatu kuu. Sehemu ya kwanza yahusu sera ya serikali ya Kenya ya

kikoloni na ile ya Kenya huru ilivyoathiri uimarikaji wa Kiswahili. Pili, ni kuhusu namna uwezo wa serikali ulivyoathiri maendeleo na uimarikaji wa Kiswahli katika kipindi tulichokijadilia. Na tatu, tumegundua kuwa wazungumzaji wa lugha fulani wanaweza kuitumia lugha hiyo na kujaribu kadiri ya uwezo wao kuipa mwelekeo wa kimaendeleo na uimara; lakini kiuwezo hili haliwezekani. Basi suala la uwezo wa wazungumzaji pia laweza kushughulikiwa na watafiti ili waweze kutoa kauli ikiwa kuimarika kwa Kiswahili kuko katika uwezo wa wazungumzaji wake au la.

Hii migao tuliyoitoa hapa ni ya kijumla mno. Watafiti wana uhuru wa kuikatakata ili kuipa migao mingine zaidi. Pia kutokana na mikondo na mielekeo ya mijadala tuliyoitoa, watafiti wanao uhuru wa kuzuka na mada nyingine nyingi.

Kazi yetu imewamba kipindi kirefu cha historia ya lugha nchini Kenya. Nia ya hali hii hasa ni kuonyesha kuwa ni muhimu pawe na sera wazi kuhusiana na malengo ya taifa lo lote kama utekelezaji wa mipango yake utafaulishwa. Kutokana na mjadala wetu kuhusu lugha nchini Kenya tuna imani kuwa ikiwa nchi hii itahusianisha suala la sera ya lugha katika mipango yake ya kipindi kifupi na pia kile kirefu, utafiti huu utasaidia katika uendelezaji wa Kenya katika ujumla wake. Utafiti huu utampa msomaji fununu

kuhusu faida za kuwa na sera wazi katika lo lote lifanywalo.

Mbali na kuwa kazi hii inaweza kusaidia wapangaji na watekelezaji wa sera zihusuzo lugha, ni imani yetu kuwa kazi kama hii inaweza kutumika kufunzia Isimu-jamii katika vyuo kwa kuwa imezua mijadala kemkemu. Tunaamini kuwa vyuo ni mahali ambapo watu hawafuati mantiki zilizopo bali hubuni, kwa mijadala motomoto, mambo mapya muradi wawe na namna ya kutetea kauli zao. Hivi ndivyo ilivyo kazi hii. Pia kazi hii inaweza kutumika katika Isimu-anthropolojia ili kujadili masuala kama vile uwezo wa lingua franka na pia kueleza namna tofauti katika hadhi zipewazo tamaduni fulani zinaweza kuathiri maendeleo ya lugha, kwa kurejelea Kiswahili nchini Kenya.

Kuna sababu nyingi zifanyazo watu kuzishughulikia lugha za Kiafrika. Kwetu sababu kuu ni ile inayohusu kuregesha kwa heshima ya watu wazungumzao lugha hizi. Tunaamini kuwa kuisoma kazi hii inayozungumzia namna Kiswahili kilivyojiimarisha katika hali ambamo kilikuwa kimewekewa vikwazo vya kubana matumizi yake kutawatia moyo waongeaji wa lugha hii pamoja na wa lugha nyingine za Kiafrika kujua kuwa lugha zao zina uwezo wa kuwasilisha cho chote watakacho bila kukwama.

# BIBLIOGRAFIA


Alexandre, P (1972) : An Introduction to Languages and and Language in Africa, N.W. University Press, Evanston, USA and Heinemann Educational Books Ltd.

Bakari, M (1978): 'Language and Nationality' katika Institute of African Studies, University of Nairobi, Staff Seminar Nos 81 - 99.

Bogonko, S. N. (1988): 'Kiswahili and Independence in East Africa' katika Bottlenecks to National Identity: Ethnic Cooperation Towards Nation Building. Professor's World Peace Academy of Kenya. Ongong'a, na Gray, K. R. (Wahariri)

Carew, J. G. (1984): 'Language and Survival' katika BIM Vol. 17, No.68, July 1984, Coles Printery Ltd, St. Michael, Barbados.

Cooper, R.L. (1976): 'Government Language Policy' katika Language in Ethiopia kilichohaririwa na Bender, L.M., OUP, Ely House, London, W.I.

Dale, P. S. (1976): Language Development: Structure and Function. Holt Rinehart and Winston, U.S.A.

Davies, C ( ? ) 'Language, Identity, and Ethnic Jokes about Stupidity' katika "International Journal of the Sociology of Language", Mahador, L.A. (Mhariri). Krips Repro, Meppel - Netherlands.

Dutton, T.E.(1976) 'Language and National Development - Long Wanem Rot?' University of Papua New Guinea.

Fabian, J (1986): Language and Colonial Power: The Appropriation of Swahili in the Former Belgian Congo 1880 - 1938. Cambridge University Press.

Falk, J. S. (1973): Linguistics and Language: A survey of Basic Concepts and Applications, Xerox College Publishing, U.S.A.

Fishman, J.A. (Mhariri) (1972): Advances in the Sociology of Language, Monton - The Hague, Paris.

―――――――― Readings in the Sociology of Language, Monton, The Hague, Paris.

Flower, F.D. (1966): Language and Education. Longman, Green and Co. Ltd.

Gleason, H.A. (1955): An introduction to Descriptive Linguistics. Holt, Rinehart and Winston, Inc. U.S.A.

Gorman, T.P. (1974): 'The Development of Language Policy in Kenya with Particular Reference to the Educational System' katika Whiteley, W.H.: Language in Kenya, OUP, Nairobi.

Gould, J.(Mhariri) (1976): A Dictionary of the Social Sciences, Tavistock Publications Ltd.

Haugen, E.I. (1966): Language Conflict and Language Planning. Harvard University Press, Cambridge, Massachussets.

Mazrui, A.A. (1972): Cultural Engineering and National Building in East Africa. N. Western University Press, Evanston Illinois.

Mkangi, K (1984): 'The Language and Political Economy' katika MWAMKO, Jarida la Kiswahili Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mutahi, K.E.(1977): 'Development of Multilingualism in Kenya' katika Historia Association of Kenya Annual Conference Papers 1977.

——————(1980) 'Language and Politics in Kenya 1900 - 1978', Makala ya Semina, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Obote, M ( ? ): 'Language and National Identification', kiambatisho A katika Mazrui, A.A (1975): The Political Sociology of the English Language, Mouton and Co. The Hague, Netherlands.

Open University, Language and Learning Course Team, Language and Social Reality. Mtayarishi wa makala ni Esland, G., Open University Press.



UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

Osundare, N (1981): 'Caliban's Curse: The English Language and Nigeria's Under-development' katika 'UFAHAMU: Journal of the African Activist Association, 10th Anniversary Issue, Vol. XI, No.2.'

Pemberton, A (1984): 'Class Conflict and Social Control in the Establishment of the Australian Welfare State: Some Neglected Questions' katika "The Australian Journal of Politics and History" Vol.30, NO.1

Stringer, D (1973): 'Language Variation and English' The Open University Press, Buckinghamshire.

Wallwork, J.F (1978): Language and People. Heinemann Educational Books Ltd, London.

Westermann, D (1934): The African Today. OUP, London.

Whiteley, W.H.(1969): Swahili: The Rise of a National Language. Methuen and Co. London.

Wyld, H.C. (1907): The Growth of English John Murray (Publishers) Ltd.



UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY